# TATHMINI LINGANIFU YA KIJINSIA YA UMILISI WA KIISIMU WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA PILI KWA SHULE ZA SEKONDARI: UCHUNGUZI KIFANI KUTOKA MUFINDI

**ALEX TAGALILE**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2022**

## UTHIBITISHO

Aliyeidhinisha hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa; **Tathmini Linganifu ya Umilisi wa Kiisimu wa Kiswahili kama Lugha ya Pili kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari: Uchunguzi kifani kutoka Mufindi** na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya utahini wa shahada ya uzamili (MA. KISWAHILI) katika isimu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

………………………..………..

Dkt. Zelda Elisifa

(Msimamizi)

Tarehe ………………………

## HAKI MILIKI

Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kuigwa, kukaririwa, kunakiliwa, kuhifadhiwa kwa njia yoyote iwayo au kuhawilishwa kwa mbinu yoyote ile; ya kielektroniki, kunakili, kurudufu katika hali yoyote bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

# TAMKO

Mimi, **Alex Tagalile,** natamka na ninathibitisha kwamba tasnifu hii inayoitwa: *Tathmini Linganifu ya Kijinsia ya Umilisi wa Kiisimu wa Kiswahili kama Lugha ya Pili Baina Wanafunzi wa Shule za Sekondari: Uchunguzi kifani kutoka Mufindi* ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

………………………………..

Alex Tagalile

Tarehe…………………….………..

## TABARUKU

Kazi hii naitabaruki kwa wazazi wangu wapendwa kwa kunisomesha hadi kufikia kiwango hiki cha elimu.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu na mwenye rehema nyingi aliyenijalia uhai, nguvu, fikra na uwezo wa kuandika na kukamilisha kazi hii.

Pili Shukurani zangu za pekee zimwendee msimamizi wangu wa utafiti huu, Dk. Zelda Elisifa kwa moyo wake wa kunihimiza na kubeba jukumu la kusimamia vyema kazi hii. Ninamshukuru kwa Uzoefu wake binafsi, uvumilivu, upendo, hekima na ushauri wake mkubwa wa kunihimiza kila nilipoona ugumu na kuchelewesha kazi

Tatu, kwa moyo mweupe napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Idara ya Isimu na Taaluma za Fasihi na wahadhiri wote waliotumia muda wao kunifundisha wakiongozwa na Mkuu wa Idara Dkt Dunlop Ochieng na Dkt. Mohamed Omary Maguo kwa mchango wao wa kitaaluma na ushirikiano walionipa kukamilisha kazi hii.

Nne, shukurani zangu ziwaendee watafitiwa wote kwa kunipa data zilizofanikisha malengo ya utafiti huu, Mungu awabariki wote.

Mwisho, nawashukuru wote walishiriki kwa namna moja au nyingine kwa hali na mali katika kuifanya kazi hii ifikie hatua hii ya ufanisi. Asanteni sana.

# IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kufanya tathmini linganifu ya umilisi wa isimu ya Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981), ili kuweza kutimiza malengo ya utafiti huu na pia kujibu maswali ya utafiti huu. Data zilikusanywa kwa njia ya jaribio la umilisi na dodoso. Eneo la utafiti lilikuwa wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa kwenye shule za sekondari tano za serikali. Watafitiwa walikuwa ni wanafunzi kidato cha tatu 115, wasichana 60 na wavulana 55 walioteuliwa kinasibu. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kitakwimu. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa wanafunzi wa kike wana ujuzi na ubobezi juu zaidi ya wale wa kiume katika nyanja nyingi sana za kiisimu zilizopimwa. Hali kadhalika utamalaki huu wa wanafunzi wa kike umeonekana katika vichocheo viliyoonekana kusababisha ufanisi wa umilisi isimu isipokuwa ukaririshaji wa yaliyofundishwa darasani, ambayo ni kikwamizo cha umilisi katika lugha, na ambamo wavulana ndio waliotamalaki kiidadi. Hata hivyo, makundi yote mawili yalifanana katika kukataa kwamba utoshelevu wa vitabu darasani ni kichocheo cha umilisi isimu ya Kiswahili kwao. Utafiti ulifikia hitimisho kuwa kuna utofauti mkubwa wa kijinsia katika umilisi wa lugha kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili na kuwa jinsia ya kike ndiyo yenye fanaka zaidi. Tumependekeza uboreshaji wa pedagojia ya Kiswahili na tafiti linganishi zifanyike pia kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni na pia kuhusu umilisi katika wigo wa Kiswahili cha mazungumzo.

**Maneno Makuu:** *Umilisi*, *Isimu*, *Kijinsia*

# YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................... ii
HAKI MILIKI........................................................................................... iii
TAMKO.. ................................................................................................ iv
TABARUKU ............................................................................................ v
SHUKRANI ............................................................................................. vi
IKISIRI…. .............................................................................................. vii
YALIYOMO ........................................................................................... viii
ORODHA YA MAJEDWALI ..................................................................... xi
ORODHA YA VIELEZO .......................................................................... xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .................................................. 1**

1.1 Usuli wa Mada ........................................................................ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ...................................................................... 5
1.3 Malengo ya Utafiti .................................................................. 7
1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti .............................................................. 7
1.3.2 Malengo Mahususi .................................................................. 7
1.4 Maswali ya Utafiti .................................................................. 7
1.5 Umuhimu wa Utafiti ............................................................... 8
1.6 Mawanda ya Utafiti ................................................................ 8
1.7 Hitimisho ................................................................................. 9

**SURA YA PILI : MAPITIO YA KAZI TANGULIZI ............................ 10**

2.1 Utangulizi ............................................................................... 10
2.2 Dhana ya umilisi wa Lugha ...................................................... 10

2.3 Dhana ya Umilisi wa Lugha....................11
2.4 Dhana ya Upimaji wa Umilisi....................13
2.5 Mapitio ya kazi Tangulizi....................15
2.6 Kiunzi cha Nadharia....................18
2.7 Pengo la Utafiti....................22
2.8 Hitimisho....................22

**SURA YA TATU : MBINU ZA UTAFITI....................23**

3.1 Utangulizi....................23
3.2 Usanifu na Mkabala wa Utafiti....................23
3.3 Eneo la Utafiti....................24
3.4 Sampuli na Usampulishaji....................24
3.4.1 Sampuli....................24
3.4.2 Usampulishaji....................25
3.5 Mbinu za Kukusanya Data....................25
3.5.1 Jaribio la Umilisi....................26
3.5.2 Mbinu ya Hojaji....................26
3.6 Maadili ya Utafiti....................27
3.7 Uchambuzi wa Data....................27
3.8 Muhutasari wa Sura....................28

**SURA YA NNE : UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA....................29**

4.1 Utangulizi....................29

4.2 Ubobezi Linganifu wa Kiswahili kama lugha ya pili Baina ya Wanafunzi wa Kike na wa Kiume wa Shule za Sekondari....30
4.2.1 Tathmini binafsi ya Ujuzi au Ufahamu wa Lugha ya Kiswahili....31
4.2.2 Umilisi Halisi wa Kiisimu ya Kiswahili....33
4.2.2.1 Umilisi katika Kutambua na Kubaini Aina za Maneno....33
4.2.2.2 Uwezo wa Wanafunzi katika Matumizi ya Msamiati na Usanifu wa Lugha....36
4.2.2.3 Utambuzi wa Matumizi ya Nafsi katika Tungo....39
4.3 Vichocheo na Vipingamizi vya Umilisi Uliobainika....43
4.3.1 Mbinu za kujifunza kama Kichocheo au Kikwamizo....44
4.3.2 Tathmini ya Ufundishaji na Utoshelevu wa Vifaa vya Kufundishia....46
4.3.3 Utayari wa Kuwasiliana kwa Kiswahili....48
4.4 Hitimisho....50

**SURA YA TANO : MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO....52**
5.1 Utangulizi....52
5.2 Muhtasari wa Utafiti....52
5.2.1 Muhtasari wa Jumla....52
5.2.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti....53
5.3 Hitimisho....55
5.4 Mapendekezo....55
5.4.1 Mapendekezo ya Jumla....55
5.4.2 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo....56
**MAREJELEO....57**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.1: Idadi ya Wanafunzi wa Kidato cha Tatu Katika Shule Lengwa .........29

Jedwali 4.2: Matokeo Kubaini na Kutambua Aina za Maneno...............................34

Jedwali 4.3: Matokeo Linganishi ya Matumizi ya Msamiati Sahihi na Usanifu wa Lugha ....................................................................37

Jedwali.4.4 : Ufaulu katika Viwakilishi Nafsi ........................................................40

Jedwali 4.5: Ufaulu wa Kimadaraja katika Utambuzi wa Nafsi .............................42

Jedwali 4.6: Majibu Kuhusu Mbinu za Ujifunzaji .................................................44

## ORODHA YA VIELEZO

Kilelezo Na. 4.1 : Mchanganuo wa Kiasilimia ya Walioshiriki Utafiti ...............30

Kielelezo Na.4.2: Tathmini binafsi ya Ufahamu au Ujuzi wa Lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili .................................................31

Kielelezo Na.4.3: Matokeo ya Ufaulu kwa Ngazi za Upimaji.............................35

Kielelezo Na. 4.4: Ufaulu katika Msamiati Kimadaraja.....................................38

Kielelezo Na. 4.5: Ujumla Linganishi Ufaulu Kimadaraja..................................41

Kielelezo Na. 4.6: Maoni Kuhusu Mbinu za Ufundishaji na Utoshelevu wa Vifaa vya Kufundishia......................................................47

Kielelezo Na. 4.7: Maoni kuhusu Nafasi ya Mbinu za Kujifunza Lugha .............49

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu umejikita katika upimaji wa ufahamu wa kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Sera ya elimu (2011:38) inaeleza kuwa, lugha ni chombo cha mawasiliano na nyenzo muhimu ya kupata mbinu-tambuzi, maarifa, teknolojia, mitazamo na maadili. Lugha huwa chombo cha kubadilisha maadili, mielekeo na matarajio ya watu walio na utamaduni unaowatambulisha (Trudgil, 1983).

Ulimwenguni kote, lugha huchukuliwa kuwa sehemu muhimu katika maisha ya mwanadamu kwani huwawezesha watu kuwasilisha hisia zao na mambo wanayoyapenda na wasiyoyapenda (Crystal, 1997) na ni chombo cha kubadilisha maadili, mielekeo na matarajio ya watu walio na utamaduni unaowatambulisha (Trudgil, 1983).

Ulimisi wa lugha yoyote ni muhimu ili kuweza kuitumia. za kukadiriwa kwa namna nyingi. Kadiri ya Chomsky (1965), umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile: Kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji hufaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha ipasavyo. Newmark (1966) anadokeza kuwa kumiliki sheria za kimsingi za lugha, umilisi wa usemaji, umilisi wa isimujamii kati ya mengine mengi ni baadhi ya mambo ambayo mtu lazima ajue ili aweze kuwa na umilisi wa kiwango cha wastani au cha juu. Naye Stern (1983) anadai kuwa viwango

vya umilisi katika lugha yoyote ile huwa tofauti kulinga na msemaji wa lugha hiyo. Ili isemekane kuwa mtu ana umilisi wa kiwango cha juu cha kiisimu katika lugha, sharti mtu huyo awe na uwezo wa kuunda maneno na sentensi katika lugha hiyo. Vilevile aweze kuitumia lugha hiyo ipasavyo katika matumizi ya kila siku na stadi nne za lugha ambazo ni: Kusoma, kusikiliza, kuzungumza na kuandika.

Mawazo haya yanashabihiana na yale ya Richard na Rodgers (1986) wanaosema kuwa, mtu kuwa na kiwango fulani cha lugha sio lazima amiliki sheria za lugha pekee bali aweze kutumia sheria hizo katika utendaji (yaani katika mazungumzo na maandishi).

Utafiti huu utajikita katika umilisi wa lugha ya Kiswahili katika muktadha wa malengo ya ubobezi katika vipengee vilivyowekwa bayana katika muhtasari wa somo la Kiswahili kwa shule za sekondari nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:1-2), ufundishaji wa somo la Kiswahili katika elimu ya msingi umelenga kumwezesha mwanafunzi:

a) kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili
b) kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali.
c) kutumia Kiswahili kupata maarifa, stadi na mwelekeo wa kijamii, kiutamaduni, kiteknolojia na kitaaluma kutoka ndani na nje ya nchi.
d) kukuza stadi za mawasiliano ili kumwezesha mwanafunzi kumudu maisha yake
e) kujenga msingi bora na imara wa kujifunza kwa ajili ya elimu ya juu na kujiendeleza binafsi kwa kutumia lugha ya Kiswahili.
f) kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Taifa.

Kwa hali hiyo, hayo ndio matarajio ya kiwango cha ufahamu wa lugha kwa wanafunzi pindi wamalizapo shule za sekondari. Ili kuhakiki ufikiwaji wa malengo hayo upimaji ni wa muhimu sana.

Babyegeya (1998) anafasili upimaji kama mchakato wa kutafuta na kupata ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa au stadi katika kiwango fulani cha elimu na kiwango hicho hutambulishwa na kufafanuliwa katika namba hasa asilimia. Mchakato wa upimaji hujumuisha mazoezi anayoyapata mwanafunzi na kuyafanya na kwa kuangalia alama alizopata katika mazoezi au majaribio husika. Nao TET (2006:2) wanaeleza kuwa upimaji katika elimu ni tendo la kutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi amejenga uwezo, amepata maarifa au amejenga stadi tarajiwa kufuatana na malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa mada za masomo yaliyopo kwenye mtaala. Katika elimu, upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi hufanywa ili kujua maendeleo na hasa kujua ni kwa kiasi gani amejenga uwezo, stadi na maarifa. TET (2005:15) wanaongeza kuwa zipo aina zifuatazo za upimaji wa wanafunzi: Upimaji wa awali, upimaji endelevu, upimaji tatuzi/gunduzi na upimaji wa mwisho/tamati. Upimaji wa awali ni upimaji ambao unapima uwezo wa mwanafunzi alionao wa kumudu kuanza kozi au mafunzo ya ngazi fulani na pia husaidia kuabinisha kama mwanafunzi ana tatizo lolote linaloweza kumkwamisha katika kujifunza kwake. Upimaji huu mara nyingi hufanyika mara tu mwanafunzi anapofika shuleni kwa mara ya kwanza kwa lengo la kuangalia na kuona ni kiwango gani mwanafunzi ana ujuzi wa kuanza masomo pia itamsaidia mwalimu kuelewa mwanafunzi ana stadi zipi na anapaswa kuanzia wapi katika kujifunza. Aina ya pili ya upimaji ambao ni upimaji endelevu ambao hufanyika wakati wote mwalimu anapofundisha ndani na

nje ya darasa. Upimaji huu unasaidia kujua maendeleo ya mwanafunzi yanayochangia kuonesha nafasi yake katika mtihani wa kumaliza muhula, mwaka na kumaliza ngazi ya elimu kama vile elimu ya awali na msingi zana zinazotumika katika kufanya upimaji huu ni pamoja na mazoezi ya darasani, majaribio, orodha hakiki na mtihani mdogo (chokozo). Aina ya tatu ya upimaji ni upimaji tatuzi/gunduzi, ambao ni upimaji unaobainisha matatizo waliyonayo wanafunzi na kutafuta mbinu za kuweza kuyatatua na kuweka mpango maalumu wa kuboresha ufundishaji. Upimaji wa mwisho/tamati hufanyika mwisho mwa kozi au mafunzo fulani lengo lake likiwa ni kujua iwapo mwanafunzi amepata maarifa, stadi na mielekeo kwa kuzingatia nyanja kama ilivyoorodheshwa katika muhtasari wa somo husika.

Sera ya elimu na mafunzo (2014) inaelezea kuwa lengo ni kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Na pia inatamka kuwa, Serikali itaweka mfumo wa upimaji na tathmini katika elimu na mafunzo utakaozingatia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa kila siku wa maendeleo ya mwanafunzi na mitihani ya mwisho ya kukamilisha ngazi husika ya elimu na mafunzo kulingana na mitaala iliyopo katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Kwa upande wa muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:4), upimaji unafafanuliwa kuwa ni kipengele muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa somo la Kiswahili utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika elimumsingi. Upimaji huu utamwezesha mwalimu kupima umahiri wa mwanafunzi kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali, kusikiliza, kusoma kwa ufasaha, kutafsiri, kujibu maswali ya habari, kuandika sentensi, habari fupi na

hadithi kwa kuzingatia kanuni za uandishi.Aidha utamwezesha mwalimu kubaini uwezo wa wanafunzi kwa kutumia msamiati sahihi katika miktadha mbalimbali. Hii ni kwa vile, kadiri ya Carell (1989), mtu anayefahamu lugha na kuwa na umilisi wa kiisimu katika lugha hiyo huonekana kuwa na ufunguo wa kufanikiwa katika masomo yake ya kitaaluma.

Mcmanara (2000) naye anasema kuwa kimsingi, mitihani ya umilisi wa mawasiliano yafaa kupima uwezo wa mzungumzaji katika kiwango cha sheria za lugha na vile vile katika kiwango cha utendaji wa lugha. Hata hivyo, mitihani mingi ya umilisi wa mawasiliano hujikita katika kupima umilisi wa kiisimu ambao huchukuliwa kama msingi wa kufahamu lugha yoyote ile. Hata ingawa umilisi wa kiisimu haumaanishi kuwa mzungumzaji ana umilisi wa kutosha katika mawasiliano. Umilisi huu wa kiisimu ndio msingi ama nguzo ya umilisi wa mawasiliano.

Kipengele ambacho utafiti huu utakishughulikia ni kile cha upimaji wa ufahamu na kutathmini umilisi wa isimu ya Kiswahili kwa kulinganisha wanafunzi kike na wa kiume wa shule za sekondari.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Umilisi kiisimu unaonekana kama msingi ama nguzo ya umilisi wa mawasiliano. Kulingana na Nunnan (2003), mtu ambaye anasitasita katika mazungumzo huonyesha umilisi wa kiwango cha chini katika lugha husika.Vilevile kuonyesha matamshi mabaya ya maneno, kuchanganya na kuhamisha misimbo, kutofuata ruwaza maalumu katika mazungumzo, kiimbo kibaya, na ung’amuaji wa maana ya maneno ni baadhi ya vigezo ambavyo huonesha badiliko la umilisi wa kiisimu katika lugha. Hata hivyo mtu anaweza kuonesha upungufu huu ikiwa umilisi wake ni wa

kiwango cha chini. Lakini anapozidi kusoma na kuimarika umilisi wake unaimarika na kisha anafuata sheria kamili za lugha. Kwa mantiki hiyo ni muhimu kupima kiwango cha umilisi kwa wanaoamili Kiswahili kama lugha ya pili. TET (2005:2-3) wanaeleza kuwa upimaji ni muhimu kwa kuwa, huamsha ari ya watoto kujifunza zaidi kujua maendeleo ya wanafunzi kiakili, kimwenendo, kitabia na kistadi, kumpa mwalimu mwelekeo wa kuboresha ufundishaji, kutoa taarifa ya maendeleo kwa wazazi au walezi na kutoa taarifa za maendeleo ya elimu kwa taifa. Kwa hiyo upimaji humuonyesha anayejifunza ni mahali gani amefanikia na ni mahali gani ana mapungufu.

Kadiri ya Muhtasari wa Kiswahili (1996:V), baadhi ya malengo ambayo ndio dira kwa mafundisho yanayotolewa shuleni juu ya lugha ya kufundishia ni pamoja na kuwa wanafunzi wanapomaliza elimu ya msingi watakuwa ni wenye maarifa, ujuzi na stadi za msingi za mawasiliano kusoma, kuandika, kuandika na kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali. Sera ya elimu (2014:20) inaeleza kuwa, lengo la jumla ni ‘kuwa na watanzania walioelimika na wenye maarifa na ujuzi kuweza kuchangia kwa haraka katika maendeleo ya Taifa na kuhimili ushindani. mapitio tangulizi yanaonyesha kuwepo kwenye nyanja za athari za lugha tangulizi katika kuamilia lugha ya pili (mf. Kamau, 2001 ; Otiende, 2014, Babusa, 2010, Chomna, 2013 ; nyanda, 2015 ; Vicent, 2018 ; Mramba, 2015 & Fauziati, 2015) na katika usukusi na uchanganuzi wa makosa (mf.Ng’ong’a, 2001 ; Wei, 2008 ; Joy, 2012 ; Obara, 2014 ; Mbula, 2011; Kisakwa, 2014). Katika kutafiti umilisi wa kiismu, kuna watafiti waliojikita katika wanafunzi wa vyuo vikuu (mf. Essa, 2001 ; Patrick, 2017) na kwa waalimu wa lugha husuka (mf. Ramadhani, 1998 ; Jokey, 2007).

Hata hivyo kumekuwa na uhaba wa tafiti linganifu kulinganisha wasichana na wavulana ili kuona kama jinsia ya muamiliaji wa Kiswahili ni kigezo cha utofauti katika ufanisi wa umilisi katika lugha la pili. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ulifanyika kwa lengo la kufanya tathmini linganifu ya umilisi wa isimu ya Kiswahili kama lugha ya pili baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume wa shule za sekondari, wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na lengo kuu na malengo mahsusi.

### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini ulinganifu uliopo katika umilisi wa kiisimu wa Kiswahili kama lugha ya pili baina ya wanafunzi kike na wa kiume wa shule za sekondari.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

i. Kupima utofauti au mfanano wa umilisi wa isimu ya Kiswahili kama lugha ya pili baina ya wanafunzi kike na wa kiume wa shule za sekondari.
ii. Kutathmini kichocheo au kikwamizi cha utofauti au mfanano wa kijinsia wa kiumulisi uliobainika katika lengo na. 1 hapo juu.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Ili kufikia malengo hayo hapo juu, utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo :

i. Ni kwa kiwango gani wanafunzi wa kike na wale wa kiume wa shule za sekondari hutofautiana au kufanana katika umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili ?

ii. Ni nini kichocheo au kikwamizi cha utofauti au mfanano kijinsia uliobainika katika lengo na. 1 hapo juu ?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa na umuhimu kwa wadau wa elimu kama ifuatavyo:-

i. Kwa upande wa nadharia ya ujifunzaji lugha, utafiti huu utatoa mchango wa namna jinsia ilivyo kisababishi cha utofauti wa umilisi wa lugha ya kiswahili kama lugha ya pili katika mazingira ya Kitanzania.

ii. Kwa upande wa walimu, utafiti huu utawasaidia kutambua kiwango cha uelewa wa mwanafunzi kwa yale waliojifunza na kurekebisha zana za kufundishia na kujifunzia.

iii. kubaini matatizo wanayopata wanafunzi wanapojifunza na kuyatafutia ufumbuzi.

iv. kurekebisha mbinu za kufundishia na kujifunzia ili kuleta ufanisi wenye mwelekeo wa kuleta ujenzi wa maana zaidi.

v. Utafiti huu utasaidia kuandaa mada na maswali ya kujipima mwanafunzi yanayoendana na uhalisia wa viwango vya utofauti wa umilisi na changamoto katika umilisi wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili.

## 1.6 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu upimaji wa umilisi wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa shule za sekondari Tanzania. Utafiti huu ulilenga kuona kiwango cha umilisi walicho nacho wanafunzi wa kike na wa kiume katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo utafiti huu umejikita katika nyanja za kiisimu katika umilisi aina za

maneno, msamiati, na viwakilishi nafsi. Pia utahusu wanafunzi wa shuke za sekondari pekee na hautahusika na walio chini au juu ya kiwango hicho cha elimu.

## 1.7 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza vipengele mbalimbali vya utafiti ambavyo ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti ambayo ni lengo kuu na lengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja na hitimisho.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imehakiki na kutathimini mapitio ya kinadharia ya kazi tangulizi. Sura hii imeonesha mtazamo wa watalaamu mbalimbali ulimwenguni kuhusiana na mada hii ya umilisi wa lugha. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi, inafuatiwa na sehemu ya pili, ambayo ni mapitio ya kitaaluma ya kazi tangulizi na sehemu ya mwisho ni hitimisho. Aidha, pengo la utafiti na kiunzi cha nadharia vimeonyeshwa ndani ya sehemu hii.

## 2.2 Dhana ya umilisi wa Lugha

Kabla ya kuongelea juu ya lugha fulani, ni jambo la muhimu kuelewa kwanza fasili ya uamili lugha. Kwa mujibu wa Chomsky (1957), binadamu huzaliwa akiwa na uwezo wa lugha, yaani kwenye ubongo wake ana mfumo ambao huzaliwa nao kwa ajili ya kujifunza lugha. Mara anapoanza kuishi katika jamii ndipo huanza kuibua sauti hizo katika mazingira bila mwenyewe kutarajia na kuanza kuzitafutia maana.

Wataalamu mbalimbali wameongelea juu ya uamiliaji lugha. Krashen na Tracy (1983) wanauona uamiliaji lugha kama mchakato unaotokea katika nafsi iliyofichika akilini mwa mtu ambayo ndiyo imuongozayo kuongea au kuandika kwa urahisi. Hivyo wao wanaona kuwa uamiliaji hujitokeza kwa mtu katika hali ya ung'amuzi bwete pasipo mhusika mwenyewe kujitambua. Kwa upande wa watoto wachanga, Jean (1992:123) anasema kuwa katika uamiliaji lugha watoto wachanga wanakuwa makini katika lugha tangu wanapozaliwa. Wanaanza kutoa maneno yanayotambulika katika kipindi cha miezi 12 hadi 15 na kuanza kuyaunganisha maneno hayo kuanzia

miezi 18. Anaendelea kufafanua kuwa watoto wote wasio na matatizo ya kimaumbile na baadhi wenye matatizo wataanza kuongea ikiwa watasikia lugha ikizungumzwa katika mazingira waliyomo.

Massamba (2004) anasema kuwa ujifunzaji lugha ni utaratibu wa kufanya jitihada rasmi za kuijua na kuitumia lugha fulani. Mtu yeyote ana uwezo wa kujifunza lugha na kuifahamu ikiwa tu atakuwa na akili timamu pamoja na ala sauti zote zinazohusiana na ujifunzaji lugha kikubwa tu ziwe hazijaathiriwa au kuathirika.

### 2.3 Dhana ya Umilisi wa Lugha

Umilisi ni ujuzi wa sheria na kanauni zinazoongoza au kuratibu matumizi ya lugha kwa usahihi. White (1959) anasema kuwa mtu binafsi ana umilisi katika shughuli fulani ikiwa ana uwezo wa kutatua matatizo katika shughuli hiyo. Umilisi wa kiisimu ni utaratibu wa kielimu katika isimu ya lugha inayomiliki wa na wanajamii lugha. Mtu kusema kuwa ana umilisi katika lugha fulani lazima awe na ufasaha wa kiwango fulani. Chomsky (1965) aliipa dhana hii ya umilisi wa lugha umuhimu zaidi alipozungumza kuhusu umilisi na utendaji. Kulingana na Chomsky wanajamii lugha huwa na ujuzi wa kuelewa mipango na matumizi ya sentensi na sheria katika lugha husika.

Hymes (1971) anaendeleza mawazo ya Chomsky kwa kuongezea kuwa ni vyema kuchunguza umilisi wa kiisimu lakini ni bora zaidi kuchunguza jinsi mtu anavyotumia lugha hiyo. Yeye anazua wazo la umilisi katika mawasiliano, ambapo anasema kuwa unaweza kuelewa umilisi wa kiisimu wa msemaji kwa kuwasiliana naye katika miktadha mbalimbali. .

Chomsky (1986) ana mawazo yanayoshabihiana na haya, kuwa umilisi hupatikana katika matumizi ya lugha. Kwa kuelewa haya, utafiti unaweza kufahamu umilisi wa kiisimu wa mwanafunzi wakati wa kuzungumza naye ili kufahamu ikiwa umeimarika na kwa kiwango kipi.

Lehmann (2006) anafasili umilisi wa kisarufi kuwa ni kule kujua umbo la lugha na maana katika matumizi yake. Anaongeza kuwa umilisi wa mtu hukua katika maisha na ufasaha wake huongezeka jinsi anavyoimarika katika miaka na sio tu katika lugha ya kwanza lakini katika lugha ya pili na ya tatu. Coseriu (1985) naye anasema kuwa mtu huongeza umilisi wa kiisimu katika maisha anapozidi kukua na hufika viwango tofauti kwa watu tofauti. Widdowson na Henry (1973) wanadai kuwa umilisi ni uchunguzi wa uwezo wa mtu wa kujua na kutumia lugha. Umilisi wa kiisimu anauona kama si jambo muhimu kwake. Vollmer (1982) anaeleza umilisi kama kuwa na sheria na elimu ya kisarufi katika lugha husika, na kuweza kutumia sheria hizi katika mawasiliano, nao Fillmore na Charles (1979) anasema kuwa lugha katika miktadha mbalimbali huweza kupimwa kutumia vigezo vilivyokubaliwa na wanajamii katika lugha husika. Canale na Swain (1980) wanaeleza umilisi wa kimawasiliano kama uwezo wa matumizi ya lugha katika mawasiliano ya kila siku. Wao wanaeleza umilisi wa kiisimu kama shughuli ya kiusomi, wanasema kuwa ufasaha katika umilisi hupimwa kupitia lugha husika.

Canale na Swain (1980) wanadai kuwa umilisi huwa katika majukumu tofauti. Mawazo haya yanaungwa mkono na Stern (1983) anayedai kuwa weledi katika lugha ni jukumu ambalo lazima litimizwe. Msemaji wa lugha hiyo sharti awe na umilisi wa kuweza kutumia lugha vilivyo na awe mwepesi wa kuunda maneno na

sentensi. Carol (1968) anaeleza kuwa umilisi wowote wa lugha unahusisha umilisi wa kiisimu na umilisi wa utendaji katika lugha hiyo. Kwamba mtu huweza kuwa na ujuzi wa kusema lugha yoyote ile ikiwa ana umilisi wa matumizi ya lugha. Mawazo haya yanaungwa mkono na Clark (1977) anayedai kuwa mtu aliye na weledi katika lugha ni lazima awe anaweza kufahamu miundo tofauti ya kileksia, kifonolojia, kisintaksia, kisemantiki na uchanganuzi usemi katika muktadha wa kijamii.

## 2.4 Dhana ya Upimaji wa Umilisi

Upimaji wa umilisi wa kiisimu huchukua mikondo tofauti. Kuna mkondo wa jarabati ambapo ufasaha wa mwanafunzi au mwanajamii lugha husika hupimwa kwa kutumia jarabati mahsusi ambapo huwa na vipengee sita au zaidi kuhusu isimu ya lugha husika (Lehmann, 2006). Ufasaha katika lugha hupimwa kupitia umilisi wa kiisimu katika lugha hiyo.

Kwa mujibu wa Tewes (1991), jarabati ya kupima umilisi wa kiisimu katika lugha yoyote ile hufanywa kupitia mazungumzo. Mtu anapozungumza, umilisi wake hufahamika kwa namna anavyojieleza na kuweza kuendeleza mazungumzo. Kigezo cha pili kinachotumiwa kupima umilisi wa kiisimu ni ujuzi hisa wa umilisi wa lugha, na hiki ni kigezo ambacho hutumiwa na wanasaikolojia kupima welekevu au ujuzi wa mtu katika akili. Kigezo hiki hutumia ufasaha maalumu katika kuelewa umilisi wa kiisimu wa mtu. Kigezo hiki huwa na idadi ya asilimia moja hadi asilimia mia moja.

Vigezo vingine vya kupima umilisi wa kiisimu ni vile vilivyoasisiwa na Nunnan (2003) anayesisitiza kuwa, katika kupima umilisi wa kiisimu wa mtafitiwa katika lugha husika, vigezo vifuatavyo hutumika. Vigezo hivi ni vitano na hutumika wakati

wa kupima umilisi katika maandishi. Navyo ni: i) Sarufi, ii) Namna au kwa ufundi fulani wa kuitumia sarufi katika mazungumzo, iii) Kwa kusudi fulani la kuandika na kupanga mawazo yako, iv) Mshikamano wa mawazo, na v) Uhusiano kuhusu kile wanachokiandika. Kila kigezo hutuzwa alama kuanzia 1-10. Wale wanaopata alama 9-10 huwa adimu, wale ambao hupata alama 7-8 huwa vizuri sana, wale ambao hupata alama 5-6 huwa vizuri, wale ambao hupata alama 3-4 huwa wastani na wale ambao hupata alama ya1-2 huwa hafifu. Kwa ujumla mtu anayepata alama ya 9-10 katika vigezo hivi vyote husemekana kuwa na umilisi wa kiisimu wa kiwango cha juu katika lugha husika.

Kadiri ya muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:1-2), ufundishaji wa somo la Kiswahili katika elimu ya msingi umelenga kumwezesha mwanafunzi, kutumia Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali, kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Taifa. Kwa maana hiyo, hayo ndio matarajio ya kiwango cha ufahamu wa lugha kwa wanafunzi pindi wamalizapo shule. Ili kuona kama malengo hayo yamefikiwa upimaji ni wa muhimu sana. TET (2006:2) wanasisitiza kuwa upimaji katika elimu ni tendo la kutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi amejenga uwezo, amepata maarifa au amejenga stadi tarajiwa kufuatana na malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa mada za masomo yaliyopo kwenye mtaala. Katika elimu, upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi hufanywa ili kujua maendeleo na hasa kujua ni kwa kiasi gani amejenga uwezo, stadi na maarifa. Nao Muhtasari wa somo la Kiswahili (2016:4) unafafanua kuwa, upimaji ni kipengele muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji huu utamwezesha mwalimu kufahamu kiwango cha umahiri wa mwanafunzi kufahamu kanuni za kiismu za lugha ya Kiswahili na

kuizitumia kwa usahihi katika miktadha mbalimbali. Aidha utamwezesha mwalimu kubaini uwezo wa wanafunzi kwa kutumia msamiati sahihi katika miktadha mbalimbali. Rivers (1968) anashadidia kuwa utaratibu huo wa upimaji unaonyesha yale asiyoyajua mwanafunzi na yale ambayo anayajua.

## 2.5 Mapitio ya kazi Tangulizi

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu ni kuchunguza viwango vya umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Ni muhimu kuchunguza tafiti za kiisimu zinazohusiana na utafiti huu. Ni muhimu pia kujua jinsi tafiti hizi zinavyolingana na kutofautiana katika madhumuni, sampuli na matokeo ya utafiti huu.

Ramadhan (1998) alipima umilisi wa kisiimu wa walimu wa shule za msingi katika Kiingereza nchini Iraq ambapo, walimu sabini wa shule za msingi walishiriki katika utafiti huu. Matokeo yameonyesha kuwa umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia ulikuwa wa iwango cha wastani, umilisi wao wa lugha ya Kiingereza kwa ujumla ulikuwa wa kiwango cha chini na hii iliathiri umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wao. Utafiti wao huu umejikita katika waalimu na uwezo wao wa kufundisha Kingereza toauti na utafiti huu uliojihusisha na umulisi wa kiisimu ya Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Essa (2001) alichunguza umilisi wa mazungumzo katika lugha ya Kiingereza kwa walimu wa shule za msingi katika Chuo cha Elimu cha Baghdad.Walimu thelathini na sita walishiriki ambapo mtafiti alitumia mjarabu wa mazungumzo kupima umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiingereza kwa walimu hawa. Matokeo yameonyesha kuwa walimu wanapohitimu wanaonekana kuwa na kiwango cha wastani katika mazungumzo na vitengo vingine vya isimu kama vile: fonetiki, sintaksia na

semantiki. Viwango vya wastani kwa walimu wanaohitimu ni dhihirisho tosha kuwa wana umilisi wa kiisimu ambao hautoshi kuweza kufunza katika shule.

Ng'ong'a (2002) alifanya uchunguzi kuhusu umilisi wa kiisimu katika Kiingereza kwa wanafunzi wa somo la Kiingereza katika Chuo Kikuu cha Maseno, alipata kuwa wanafunzi wengi wa Kiingereza hawakuwa na welekevu katika somo hili hali wao ndio walitakiwa kwenda kufundisha katika shule za upili nchini Kenya. Wanafunzi hawa walikuwa na makosa mengi ya kisarufi, walikosa ufasaha wa lugha hii ya Kiingereza katika mawasiliano yao na walishindwa kuelewa vipengee muhimu vya kimsingi kuhusu lugha ya Kiingereza.

Jokey (2007) kwa upande wake alipima umilisi wa mazungumzo kwa walimu wa Kiingereza katika mji wa Baghdad. Walimu arobaini na tano walishiriki katika utafiti huu. Matokeo ya uchunguzi yameonyesha kuwa walimu walikuwa na upungufu katika matumizi ya lugha ya Kiingereza. Hii ilionekana katika matamshi ya maneno ya Kiingereza na walitumia msamiati usiyofaa katika sentensi wakati wa mazungumzo.

Kamau (2015) alichunguza athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu katika kaunti za Nairobi, Kiambu na Murang'a kwa wanafunzi wa shule za upili.Matokeo yameonesha kuwa lugha ya Kikuyu huathiriwa na matumizi ya Kiingereza, Kiswahili na sheng'. Utafiti huu unachunguza umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili na vilevile sampuli yetu ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno ili hali ya Kamau ilikuwa ya wanafunzi wa shule za upili. Lugha ya Kiswahili huathiriwa na lugha nyingine kama vile Kiingereza na sheng'. Athari

hizi huonekana katika matamshi na maandishi. Mtu anapozungumza athari hizi huonekana katika uundaji wa maneno na sentensi.

Criper na Dodd (1984) walifanya utafiti kuhusu lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari. Katika utafiti huo wataalamu hao walichunguza ujuzi wa lugha ya Kiingereza walionao walimu na wanafunzi katika kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari nchini Tanzania. Ili kupata matokeo ya kile walichokuwa wakikichunguza, wataalamu hao walitoa majaribio kwa wanafunzi elfu mbili mia nne na kumi kutoka ngazi zote za elimu. Matokeo ya majaribio hayo yaliwafanya wataalamu hao kugundua kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari siyo njia sahihi ya kutolea elimu katika ngazi hizo. kueleweka kwa lugha ya Kiingereza kuko chini sana takribani katika shule zote zilizofanyiwa utafiti huo. Ni dhahiri kwamba matumizi ya Kiingereza yanafanya kujifunza kuwa kugumu. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha asilimia kumi ya wanafunzi wa kidato cha nne waliofanyiwa utafiti walikuwa na uwezo mdogo wa kuelewa kitu chochote kilichofundishwa kwa lugha ya Kiingereza.

Pili, asilimia ishirini ya wanachuo waliokuwa katika kundi lilopimwa walikuwa na uwezo wa kusoma na kuelewa vitabu vya taaluma mbalimbali walizokuwa wanasomea. Msingi mzuri ama mbovu wa lugha ya Kiingereza walio nao wanachuo wa vyuo vya kati una athari kubwa katika kujifunza na kufaulu kwao katika fani wanazosomea. Kimsingi, hujifunza lakini ufanisi haujitokezi katika mazingira ambamo wanachuo hao hawaimudu hiyo lugha ya kujifunzia ambayo ndiyo nyenzo ya kufanikishia mawasiliano katika tendo la kufundisha na kujifunza.

*Kuhusu athari za lugha mama*

Kuna tafiti zilizojikita katika nafasi ya lugha mama katika umilisi wa lugha ya pili. Baadhi ya tafiti hizo ni kama ifuatavyo. Kamau (2015) alichunguza athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu katika kaunti za Nairobi, Kiambu na Murang'a kwa wanafunzi wa shule za upili. Matokeo yameonesha kuwa lugha ya Kikuyu huathiriwa na matumizi ya Kiingereza, Kiswahili na sheng'. Lugha ya Kiswahili huathiriwa na lugha nyingine kama vile Kiingereza na sheng'. Athari hizi huonekana katika matamshi na maandishi. Mtu anapozungumza athari hizi huonekana katika uundaji wa maneno na sentensi.

Chomba (2013), alifanya uchunguzi kuhusu athari za sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kiingereza. Matokeo yaliyopatikana yameonesha kuwa lugha ya Kiingereza huathiri na matumizi ya sheng' kwa wanafunzi wa shule za mji wa Nairobi. Athari hizi zimeonekana kwa maandishi na mazungumzo yao.

Kamau (2015) alifanya utafiti kuhusu athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Sheng' kwa lugha ya Kikuyu. Utafiti wake ulifanywa katika miji ya Nairobi, Kiambu na Murang'a. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa, lugha hizi tatu huathiri kwa kiwango kikubwa umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kikuyu kwa wanafunzi wa shule za upili. Hali hii huwafanya wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu. Utafiti wa Kamau ulichunguza athari za lugha ya Kiingereza, Kiswahili na sheng' kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu ilihali utafiti wetu unachunguza athari za kihehe kwa umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia moja ambayo ni Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981). ilihusika katika uchanganuzi wa data

zinazohusiana na umilisi wa lugha ya kiswahili katika vipengele vyote vilivyopimwa vyema na sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, othografia, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika.Hivyo ni dhahiri kuwa nadharia hii inao uwezo na ubora toshelevu wa kuvichanganua na kuvifafanua vipengele vyote vilivyopimwa.

Kwa mujibu wa nadharia hii, umilisi kamili unaundwa na maarifa ya lugha ya mazungumzo na lugha ya ishara katika mkakati wa mawasiliano ambao hutumika kufidia mawasiliano yaliyovunjika kutokana na kutoweka na umilisi kamili katika kipengele kimoja au zaidi vya umilisi wa lugha. Hii hujumuisha kufupisha taarifa kwa kutumia maneno ya mzungumzaji mwenyewe, kurudiarudia, kuacha baadhi ya maneno kudondosha maneno, sarufi / maana, kuhisi kubadilika kwa lahaja na aina ya uzungumzaji, kuboresha ujumbe na kadhalika.

Nadhari hii pia hushadidia kuwa ili mzungumzaji awe na umilisi wa mawasiliano wa lugha, anahitajika kuwa na mbinu za kimazungumzo na zisizo za kimazungumzo za kuhakikisha kuwa mawasiliano hayavunjiki kwa vile labda ana upungufu katika vipengele vile vingine vya umilisi wa mawasiliano kama kile cha kiisimu. Mzungumzaji lazima afahamu mbinu anazoweza kutumia ili mawasiliano yasivunjike kama vile kurudia rudia jambo, kutumia maelezo wakati amekosa neno la dhana fulani, kukwepa kutumia maneno asioyafahamu vyema kati ya mbinu nyingine”. Mzungumzaji lazima afahamu matumizi ya ishara mbali mbali anazoweza kutumia kuhakikisha kuwa mawasiliano hayavunjiki.

Kwa mujibu wa Canale na Swain (1980,1981) na Canale (1984) vipengele vya umilisi wa mawasiliano viko vinne ambavyo ni: umilisi wa kiisimu, umilisi wa kiisimujamii, umilisi wa mbinu za mawasiliano na umilisi wa uchanganuzi usemi.

Utafiti huu ulijihusisha na kipengere kimoja tu, ambacho ni umilisi wa isimu. Umilisi huu ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki katika mazungumzo. Katika mujibu wa Canale na Swain (1980, 1981), ujuzi wa kisarufi ulifasiriwa zaidi kwa kuzingatia mawazo ya Chomsky (1965) juu ya dhana ya umilisi wa lugha. Umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile kufahamu kuhusu leksia, fonetiki, othografia, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha lazima awe na uwezo wa kiutendaji katika lugha husika yaani awe na uwezo wa kutumia lugha ile katika miktadha tofauti ya kijamii kwa usahihi.

Awali, kabla ya Canale na Swain (1981), Chomsky (1957) alieleza kuwa mtu anapojifunza lugha huanzia na umilisi (ujuzi) na anaendelea kudai kuwa kwa kiasi kikubwa umilisi wanaokuwa nao wazawa wa lugha moja hufanana na hii ndiyo inayowafanya waelewane katika mazungumzo yao kwamba mzungumzaaji anasema kile anachotaka kusema na msikilizaji anaelewa kile kilichosemwa na mzungumzaji lugha moja hufanana na hii ndiyo inayowafanya waelewane katika mazungumzo yao. Mambo muhimu kwa mzawa wa lugha kuwa nayo ili awe mmilifu wa lugha.

Umilisi wa isimu kama dhana mojawapo ya msingi ina ulazima kwa mzawa wa lugha kuwa nayo kutokana na sababu kuwa humsaidia kujua miundo na aina mbalimbali za santensi katika lugha yake, kutambua sentensi sahihi na ambazo sio sahihi, zikiwa zinaandikwa au kuzungumzwa, humsaidia kutunga sentensi zenye urefu wowote, humsaidia kutambua sentensi zenye utata na Vile vile humsaidia kutambua sentensi zenye maana sawa na sentensi zenye maana na zile zisizo na maana.

Kwa kifupi, umilisi wa kiisimu ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria hizi za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki katika mazungumzo. Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain, kama ilivyofafanuliwa hapo juu, iliongoza uchambuzi wa malengo yote ya utafiti huu na ilituwezesha kupima uwezo walio nao wanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Na ilijitosheleza katika kupima ubobezi walionao wanafunzi wa shule tafitiwa za sekondari katika lugha ya Kiswahili na pia kutathimini ubobezi waliona wanafunzi dhidi ya sifa tarajali za lugha ya kufundishia na kuchambua vipengele vyote vilivyofanyiwa upimaji. Hii ni kwa sababunadharia hii humsaidia mjifunzaji kujua miundo na aina mbalimbali za santensi katika lugha husika, kutambua sentensi sahihi na ambazo sio sahihi, zikiwa zinaandikwa au kuzungumzwa, husaidia kutunga sentensi zenye urefu wowote , humsaidia kutambua sentensi zenye utata. Vile vile humsaidia kutambua sentensi zenye maana sawa na sentensi zenye maana na zile zisizo na maana.

Mtafiti alitumia nadharia hii katika kuangalia jinsi wanafunzi wanavyoweza kufuata sheria za lugha, yaani uwezo wa mzungumzaji wa kuzifahamu vyema sheria za lugha.

## 2.7 Pengo la Utafiti

Kulingana na utafiti wa mapitio ya kazi tangulizi, tafiti za umulisi wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili zilitafitiwa zaidi ktika nyanja za athari za lugha tanguliizi na katika ngazi za elimu za juu zaidi ya shule za sekondari. Hii imechangiwa zaidi na kiu ya watafiti wa umilisi lugha kujikita katika muktadha wa lugha ya kufindishia ya Kiingereza katika ngazi hizo na tafiti katika ngazi ya shule za awali na msingi. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu ulilenga kuziba pengo hili la maarifa kwa kufanya upimaji wa umilisi wa isimu kwa wanafunzi wa shule za sekondari kuona kiwango chao cha umilisi wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imejihusisha na mapitio mbalimbali ya kitaaluma na ya kazi tangulizi. Sura hii imeonesha mtazamo na tafiti za watalaam mbalimbali ulimwenguni kuhusiana na mada ya utafiti juu ya umulisi wa lugha. Katika sura hii pia tumeelezea kwa kina kiunzi cha nadharia ambacho kiliongoza uchambuzi wa data za utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulika na mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika mchakato wa kufanya utafiti. Sehemu kuu katika sura hii ni usanifu na mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, maadili ya utafiti, mbinu za ukusanyaji data, mchakato wa uchambuzi wa data na mwisho ni muhtasari wa sura.

## 3.2 Usanifu na Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kifani kwa upande wa usanifu. Aina hii ya usanifu humruhusu mtafiti kuzama zaidi katika mada anayoichunguza kwa vile watafitiwa wake na zifa zao huwa na mfanano wa karibu na pia eneo lake la kijiografia huwa ni dogo. Katika muktadha wa utafiti huu, uchunguzi kifani wetu ni wanafunzi wa shule za sekondari na ambao wote huishi wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa

Kwa upande wa mkabala wa utafiti, kuna mikabala mikuu miwili ya ukusanyaji na uwasilishaji wa data: mkabala wa kimaelezo na mkabala wa kitakwimu. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mikabala yote miwili. Mkabala wa kimaelezo, umetumika pasipo kufuata taratibu za kitakwimu kwa kutoa chanzo cha wanafunzi kuwa na umilisi katika Kiswahili kama lugha ya pili na kuzielezea data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti.

Kothari (1990), anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu. Anasema pia ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti.

Mkabala wa kitakwimu/kiidadi, umetumika kuonesha data ambazo zimefupishwa kwa namna ambayo ni rahisi kuchambuliwa na kueleweka kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu. Data hizo takwimu ni zile zinazoonesha viwango toafuti vya umilisi wa lugha kama vinavyotafsirika katika upimaji wa umilisi kwa njia ya majaribio. Matinde (2014) anasema kuwa takwimu ni njia mahsusi ya mawasiliano idhihirishayo kwa uwazi na uhakika chochote kile kinachohusika. Kwa hiyo data zilizokusanywa zimepangwa, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa. Mkoa wa Iringa una wilaya nne ambazo ni Iringa Mjini, Mufindi, Kilolo na Iringa Vijijini. Aidha wilaya ya Mufindi ina tarafa tano ambazo ni Malangali, Ifwagi, Kasanga, Kibengu na Sadani. Ifwagi ndio tarafa ambapo shule tano teule za sekondari zinapatikana.

Miongoni mwa sababu zilizopelekea mtafiti kuteua eneo hili la tarafa ya Ifwaji kufanyia utafiti ni pamoja na kuwa hakuna utafiti wowote uliofanyika katika eneo hili, aidha eneo lina uwakilishi mzuri kwani ni eneo la mbali na manispaa ya Iringa na mtafiti alipata picha halisi jinsi wanafunzi walivyo na umilisi wa lugha ya Kiswahili tofauti na maeneo ya mijini ambapo muda mwingi mawasiliano hufanyika kwa lugha ya Kiswahili. Pia tafiti nyingi zimekuwa zikifanyika katika maeneo ya manispaa na maeneo ya nje na ya vijijini kusahaulika.

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji

### 3.4.1 Sampuli

Kwa mujibu wa Mligo (2012), sampuli ni kundi fulani la watu au vitu lililoko ndani ya mkusanyiko wa watu au vitu ambao mtafiti anaamini kwamba linazo habari

zitakazomwezesha kujibu swali lake la utafiti. Kwa mantiki hiyo, kuchagua sampuli ni kuchagua kundi dogo la watu au vitu katika mkusanyiko wenye makundi ya aina nyingi kwa malengo maalumu aliyonayo mtafiti kwa ajili ya utafiti wake. Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kuwatafiti wanafunzi wote katika wilaya ya Mufindi yenye tarafa tano, tulifanya uteuzi wa sampuli ili kupata kundi dogo la watu ambao wangefanyiwa utafiti kuwakilisha kundi kubwa la wanafunzi.

Kwa mujibu wa Koul (2009), walengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kwa hiyo, katika utafiti huu kundi lengwa lilikuwa wanafunzi wa kike na wa kiume wa kidato cha tatu wa shule za sekondari katika wilaya ya Mufindi tarafa ya Ifwagi.

### 3.4.2 Usampulishaji

Kwa minajii ya kupata sampuli katika kazi ya utafiti, inampasa mtafiti kufanya mchakato wa usampulishaji, ambao hutegemea mada husika na lengo la utafiti. Kwa mujibu wa Adam (2008), usamplishaji ni mbinu, mchakato au kitendo cha kutafuta walengwa wa utafiti. Ili kufanya utafiti huu, walengwa walikuwa ni wanafunzi wa kidato cha tatu wilayani mufindi. Katika utafiti huu watafitiwa 115 (wavulana 55 na wasichana 60) waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu ambapo majina ya tarafa tano za Mufindi yaliandikwa kwenye karatasi zikakunjwa na kisha moja ikachaguliwa na ilipofunguliwa ilikuwa na jina la tarafa aya Ifwagi. Mbinu hii ilitumika pia kuwapata watafitiwa katika shule husika.

## 3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Kwa mujibu wa mada hii ya utafiti, mbinu mbili zimetumika kutupatia data ambazo ni jaribio la umilisi na hojaji.

### 3.5.1 Jaribio la Umilisi

Katika kufanikisha kukusanya data lengwa kukidhi malengo ya utafiti, kulitumika mbinu ya jaribio la utafiti katika kukusanya data zilizohusiana na kiwango cha umilisi wa lugha walicho nacho wanafunzi wa kike wakilinganishwa na wale wa kiume. Katika mbinu hii maswali yaliyolenga kupata taarifa kuhusu umilisi waliyonao makundi ya kijinsia ya wanafunzi yaliandaliwa na kisha kuhahikikiwa na wataalamu wabobezi wa upimaji katika elimu lugha, akiwepo msimamizi wangu.

### 3.5.2 Mbinu ya Hojaji

Kwa mujibu wa Kothari (2012), mbinu ya hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali au dodoso yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Aidha, Mligo (2012) anaendelea kudai kwamba, hojaji ni karatasi iliyoandikwa maswali ambayo hupewa mtafitiwa ili aandike majibu kulingana na maelezo ya wataalam hao, hojaji ni maswali yaliyoandaliwa na mtafiti kwa lengo la kumhoji mtafitiwa, na maswali haya yanafungamana na malengo ya utafiti husika, data hukusanywa kutokana na mtafitiwa kujibu maswali yaliyoorodheshwa katika karatasi.

Katika utafiti huu, hojaji ilitumika katika kukusanya na kutafuta data zilizohusiana na taarifa za awali zinazowahusu watafitiwa kama hasa jinsia zao na shule wanazosoma na pia kupata taarifa za kiwango cha tathmini binafsi ya umilisi wa lugha na maoni yao kuhusu visababishi na/au vikwamizi vya mafanikio katika umilisi wao wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

### 3.6 Maadili ya Utafiti

Ili kufanikisha utafiti huu mtafiti analazimika kufuata taratibu na kanuni za kimadili zinazoongoza tafiti hasa kupata taarifa za mtu huku uhuru na heshima yake vikiheshimiwa. Pons (1992) anasema kuwa maadili ya utafiti ni pamoja na haki ya kuwa na usiri yaani matafiti kutotoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti. Maelezo hayo yanafanana na ya Aeker (2002) kama alivyonukuliwa na Adam (2008), waliotaja maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na haki ya kuwa na usiri, yaani mtafiti kutotoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

Kwa utafiti huu, mtafiti aliomba kibali cha kufanya utafiti katoka mamlaka husika ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Pia aliomba ruhusa na kibali kutoka kwa uongozi wa shule husika ili kupata ruhusa ya kukusanya data katika shule zao na shule hizo, ili kulinda usiri wa umilisi, zipewa majina ya Kiherufi (A, B,C,D na E). Mwisho, mtafiti aliwapa wanafunzi fomu maalum ya kujaza kuridhia kufanyiwa utafiti na kupimwa kiwango chao cha umilisi.

### 3.7 Uchambuzi wa Data

Kothari (2008) anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika.Uchambuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo

na kiidadi. Mbinu hizi zilistahili kwa sababu zilitoa maelezo na kutoa ufafanuzi kuhusu viwango vya umilisi wa Kiswahili kama lugha ya pili na kutathmini kiwango cha ubobezi wa kiswahili walichonacho wanafunzi wa kidato cha tatu. Data zilihakikiwa na kupitiwa kwa makini kwa kupangwa katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti. Data za aina moja zimewekwa pamoja ili kurahisisha usomaji wa maudhui yaliyokusudiwa.

### 3.8 Muhutasari wa Sura

Sura hii imechambua mbinu za utafiti, eneo la utafiti, usanifu na mkabala wa utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data (hojaji na jaribio la umilisi wa lugha ), maadili ya utafiti na mwisho, mchakato wa uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo. Sura inayofuata inahusiana na uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

## 4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha data zilizopatikana uwandani. Data zimechambuliwa kwa kutumia misingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981) na kadiri ya mlolongo wa malengo mahususi ya tafiti.

Uwasilishaji wa data pia umefanyika kitakwimu na kimaelezo, maelezo ya kitakwimu yametolewa kwanza kisha kufautiwa na data za kimaelezo.


Baada ya kukusanya taarifa na kuzipanga pamoja, uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kuangalia takwimu ya majibu ya wanafunzi juu ya ubobezi wao katika lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa shule za sekondari na kutathmini kiwango cha umilisi wa lugha hiyo.

Watafitiwa walikuwa kama ifuatavyo

Jedwali Na.4.1 : Idadi ya Wanafunzi wa Kidato cha Tatu Katika Shule Lengwa

| **Sn** | **Shule** | **Idadi ya wanafunzi** | | | **Waliofanyiwa utafiti** | | | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KE | ME | JUMLA | KE | ME | JUMLA | |
| 1 | A | 46 | 42 | 86 | 13 | 12 | 25 | 29 |
| 2 | B | 48 | 33 | 71 | 13 | 12 | 25 | 35.2 |
| 3 | C | 39 | 37 | 77 | 11 | 9 | 20 | 32.5 |
| 4 | D | 45 | 44 | 89 | 10 | 10 | 20 | 28 |
| 5 | E | 41 | 40 | 81 | 13 | 12 | 25 | 30.4 |
| | Jumla | | | 404 | 60 | 55 | 115 | 51.3 |

Kama jedwali linavyoonesha hapo. Katika shule hizo tano kidato cha tatu wapo jumla ya wanafunzi 404. Kati ya hao wanafunzi 115 sawa na asilimia 51.3 walishiriki utafiti huu na mgawanyiko wake kiidadi haukuwa sawia kwa kila shule, kama kelelezo Na.4.1 hapa chini kinavyoooonesha.




**Kilelezo Na. 4.1 : Mchanganuo wa Kiasilimia ya Walioshiriki Utafiti**

Kama kielelezo Na.4.1 hapo juu kinavyoooonesha, washiriki katika utafiti walitofautiana shule moja na nyingine kwa vigezo vya utayari wao katika kushiriki utafiti huu. Shule A ndiyo iliyokuwa na asilimia kubwa zaidi (35.2%) ikifuatiwa na shule C yenye 33.5%. Shule ambazo washiriki wake walikuwa chini ya 30% ya idadi nzima ya wanafunzi wa kidato husika ni D (28%) na A (29%).


## 4.2 Ubobezi Linganifu wa Kiswahili kama lugha ya pili Baina ya Wanafunzi wa Kike na wa Kiume wa Shule za Sekondari

Madhumuni mahususi ya kwanza katika utafiti huu yalilenga kulinganisha umilisi wa kiisimu wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa kike na wa kiume

wa shule za msingi. Sehemu hii inawasilisha matokeo na kujadili upimaji uliofanyika kwa wanafunzi juu ya umilisi wao katika lugha ya Kiswahili.

### 4.2.1 Tathmini binafsi ya Ujuzi au Ufahamu wa Lugha ya Kiswahili

Mtafiti, kwa kutumia dodoso, aliwaelekeza watafitiwa kujifanyia tathmini ya kiwango chao cha umilisi wa lugha ya Kiswahili ambapo aliwaelekeza kuweka 1 kama wanaamini kuwa wana kiwango cha juu cha ufahamu wa lugha hiyo, 2 kama wana ufahamu wastani, 3 kama waamini wana ufahamu hafifu na 4 kama hawana hakina na ufahamu wao. Matokeo ya majibu ya wanafunzi ni kama yanavyotanabaishwa kwa kielelezo na. 4.2 hapa chini.




**Kielelezo Na.4.2: Tathmini binafsi ya Ufahamu au Ujuzi wa Lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili**

Jedwali 4.2 linaonesha watafitiwa walionesha viwango anuwai katika tathmini binafsi waliyojifanyia. Wengi wao (63, sawa na 54.7% ya watafitiwa wote) walijiona kuwa na ujuzi na ufahamu wa juu wa lugha ya Kiswahili. Kati ya hao, 41 (65%) ni wasichana na 22 (35%) ni wavulana. Watafitiwa 37 (32.2% ya watafitiwa

wote) walijitathmini kuwa na kiwango cha wastani wa umilisi wa lugha ya Kiswahili, 33 (62.2%) miongoni mwao wakiwa ni wasichana 23 (54%) na 10 (27.8%) wavulana. Kwa upande wa waliojiona wana umilisi hafifu, jumla yao walikuwa 12 (10.5%) miongoni mwao 4 (33%) wakiwa wavulana na 8 (67%) wasichana. Kundi dogo sana (wanafunzi 7 (6%) ya watafitiwa wote walisema hawana hakika. Kwa ujumla wanafunzi walio wengi walijitathmini kama wenye umilisi wa juu wa lugha ya Kiswahli, wengi wao wakiwa ni wasichana.

Van der Slik na wenzake (2015) katika utafiti wao wa mlinangano wa kijinsia katika uamiliaji wa Kidachi kama lugha ya pili kwa wahamiaji 88, aling'amua kuwa waamiaji wa kikie waliwapita wale wa kiume katika umilisi wa lugha ya Kidachi kama lugha ya pili. Vilevile utafiti wa Główka (2014) ulifanyika kupima ulinganifu katika uamiliaji wa lugha ya Kiingereza kama lugha ya kigeni kwa wanafunzi wa Sekondari na vyuo vya elimu ya juu Poland, ionesha pia kuwa wanafunzi wa kike walitamalaki katika ufaulu wa upimaji wa umilisi ukilinganisha na wale wa kiume. Hata katika kujitathmini wenyewe kuhusu ufahamu wao wa lugha, Rudzinska (2013) aling'amua katika utafiti wake kuwa wanawake walijitathmini kuwa na uwezo mkubwa sana ikilinganishwa na namna wanaume walivyojitathmini.

Mtafiti pia aliwataka watafiwa kubaini ni vigezo gani vinavyowafanya wajione kuwa wana ujuzi/ufahamu katika lugha ya Kiswahili. Watafitiwa walisema kuwa vigezo vinavyowafanya wajione kuwa wana ujuzi na ufahamu katika lugha ya Kiswahili ni kutokana na kuwa wana uwezo wa kuzungumza lugha ya Kiswahili, kusikiliza na kuelewa sentensi zinazoongelewa na watu wengine kwa kutumia lugha ya Kiswahili, kusoma maandiko na kuandika vizuri kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Aidha wana

uwezo wa kutambua maneno mbalimbali ya Kiswahili na pia kuweza kung'amua kuwa neno fulani sio la Kiswahili.

Mojawapo ya kazi fanani ni ile ya Van de Slik na wenzake (2015) waliotafiti tofauti za kijinsia katika kujitathmini umilisi wao binafsi wa Kidachi kama lugha ya pili wahamiaji 49 waliohamia Uholanzi. Matokeo ya utafiti wao yalionesha kuwa wahamiaji wa kike walionesha kuwa wanaamini wana uwezo mkubwa wa umilisi wa Kidachi kama lugha ya pili kuliko wanaume. Utafiti huu ulionekana wenye uimara kwa vigezo vya umri, muda wa kuwasili kwa wahamiaji na muda waliotumia kujifunza Kidachi. Hata hivyo hakuna utofauti ulioonekana miongoni mwa wanaume na wanawake katika stadi za kusoma na kusikiliza.

### 4.2.2 Umilisi Halisi wa Kiisimu ya Kiswahili

Utafiti huu ulienda ziada ya tathmini binafsi na kupima umilisi wa wanafunzi watafitiwa kwa kutumia jaribio la umilisi wa Isimu ya Kiswahili.

#### 4.2.2.1 Umilisi katika Kutambua na Kubaini Aina za Maneno


Katika kufikia lengo la upimali wa umilisi wa kiisimu, mtafiti alitumia jaribio la umilisi lililowaelekeza wanafunzi watambue na kubaini aina za maneno katika sentensi mbalimbali zisizokuwemo. Maswali hayo yalilenga kupima uwezo wa wanafunzi hao kutambua na kubaini aina za maneno katika sentensi mbalimbali. Majibu ya wanafunzi yaliingizwa kwenye kikokotoo cha SPSS na wastani na asilimilia za matokeo yao zilikuwa kama jedwali na.4.2 hapa chini.

**Jedwali 4.2 : Matokeo Kubaini na Kutambua Aina za Maneno**

| sn | Aina ya neno | Idadi lengwa | waliofaulu | | waliokosa | | wasiofanya chochote | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME |
| 1 | Vitenzi | 10 | 17 | 10 | 22 | 33 | 13 | 10 | 52 | 53 |
| 2 | Nomino | 10 | 20 | 17 | 13 | 27 | 22 | 16 | 55 | 60 |
| 3 | vivumishi | 10 | 42 | 28 | 17 | 13 | 7 | 3 | 62 | 53 |
| 4 | vielezi | 10 | 30 | 10 | 53 | 7 | 9 | 6 | 92 | 23 |
| **5** | **Jumla** | **40** | **109** | **65** | **105** | **80** | **51** | **35** | **261** | **189** |
| | **Wastani** | | **27.25** | **16.25** | **26.25** | **20** | **12.75** | **8.75** | **65.25** | **47.25** |

Kadiri ya data kwenye jedwali na.4.2 hapo juu, ufaulu wa ujumla kwa wastani, wasichana waliofaulu ni 27.25 (sawa na 45.4% ya wasichana wote watafitiwa) wakati wavulana waliofaulu ni wastani wa 16.25 pekee (sawa na 29.5%) ya wavulana wote watafitiwa. Ufaulu katika vivumishi ndio uliotamalaki dhidi ya makundi mengine ya aina za maneno kwani wasichana 42 (sawa na 70%) walifaulu dhidi ya wavulana ambao 28(50.9%) walifaulu. Hii inafuatiwa na vielezi ambapo pia wasichana waliongoza kwani kati ya watafitiwa 60 wa kundi hili, 30 (50%) walifaulu wakati wavulana waliofaulu vielezi ni 10 tu, sawa na 18.2% pekee. Kwa ujumla wake, vitenzi ndivyo vilikuwa na ufualu hafifu kwa makundi yote kwa kuwa na wasichana 17 (29.3%) na wavulana 10(18.2%) tu walifaulu. Yote kwa yote, wasichana wameonesha kufaulu kwa wingi zaidi ya wavulana katika kategoria zote nne za aina za maneno.

Mtafiti alitaka pia kutathmini ufaulu wa kimadaraja katika umilisi linganifu wa kiisimu baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume, amabopo kikokotoo cha excel kilileta matokeo kama Kielelezo na. 4.3 kinavyotanabaisha.




**Kielelezo Na.4.3: Matokeo ya Ufaulu kwa Ngazi za Upimaji**

Kielelezo na.4.3 hapo juu kinaonesha kwamba ufaulu kwa ujumla ulikuwa ni mzuri katika kila kategoria ya aina za meneno. Hata hivyo, wengi wa wavulana walikuwa katika ufaulu wa daraja la ‘C’hasa katika Vitenzi (25, sawa na 45.4%) na kwenye Nomino (18, sawa na 32.7%). Ufaulu huu ni wa ‘wastani’ kiashiria kuwa umilisi wa wavulana walio wengi katika aina za maneno si mkubwa sana ila pia sio dhaifu mno. Kwa upande wa wasichana, wengi wao wako kwenye ufaulu wa daraja la ‘B’ hasa kwenye Vielezi (23, sawa na 38.3%) na Nomino (19, sawa na 31.7%). Hata hivyo wasichana wengine 34 (56.7%), yaani 17 (28.33%) kwenye Vitenzi na 17 (28.33%) kwenye Vielezi) walifaulu katika daraja ‘A’ lenye maana ya ‘safi sana’. Hii inamaanisha wengi wa wasichana walikuwa kwenye ufaulu mzuri na mzuri sana kwa maana kwamba hao wanao umilisi mzuri wa kiisimu ukilinganisha na wavulana ambao ni wachache sana (12, sawa na 21.8% kwa upande wa Vielezi na 10, sawa na

18.2% kwa upande wa Nomino, wakati katika Vivumishi hakuna aliyepata daraja hilo).

Utafiti wa Sökmen (1993) kuhusu utofauti wa kijinsia katika kuhusishanisha aina za maneno, aligundua kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya wajifunzaji lugha wa kike na wale wa kiume na kwamba wanawake ndio walioonesha umilisi mkubwa zaidi. Pia utafiti huu unalandana na ule wa Alahmadi na Lahlali (2019) waliochanganua makosa katika uamiliaji wa Kiingereza kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa Kisaudi wakilinganisha wanaume na wanawake. Walijikita katika makosa katika Kiingereza cha mazungumzo. Watafiti hawa waling'amua kuwa wanafunzi wa kiume walifanya makosa zaidi ya wale wa kike ikaashiria umilisi wao hafifu katika Kiingereza cha mazungumzo.

#### 4.2.2.2 Uwezo wa Wanafunzi katika Matumizi ya Msamiati na Usanifu wa Lugha

Mtafiti alitumia jaribio la umilisi kwa watafitiwa katika matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha. Sentensi 12 za msamiati anuwai zilitumika kupima umilisi katika eneo hili la isimu. Jumla ya msamiati lengwa ulikuwa 12, 4 wa kijamii (*tafrija, mahari, msiba, kifungua kinywa*), 4 wa kibiashara (*soko, mtaji, muuzaji, mnunuzi*), na 4 wa ujenzi (*paa, daraja, seremala, samani*). Matokeo ya umilisi katika msamiati ni kama ifuatavyo katika jedwali na. 4.3.

**Jedwali 4.3: Matokeo Linganishi ya Matumizi ya Msamiati Sahihi na Usanifu wa Lugha**


| AINA YA MSAMIATI | JINSIA | WALIOPATA | WALIOKOSA | WASIOJIBU | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJAMII | KE | 38 | 21 | 1 | 60 |
| | ME | 27 | 16 | 12 | 55 |
| KIBIASHARA | KE | 51 | 6 | 3 | 60 |
| | ME | 19 | 20 | 16 | 55 |
| UJENZI | KE | 48 | 11 | 1 | 60 |
| | ME | 21 | 30 | 4 | 55 |
| **JUMLA** | | **204** | **104** | **37** | **345** |
| **WASTANI** | | **34** | **17.3** | **6.2** | **57.5** |

Kadiri ya data kwenye Jedwali na.4.3, wastani wa jumla wa waliofaulu msamiati ni 34, sawa na 29.6% ya watafitiwa wote 115 wakati waliokosa ni wastani wa 17.5, sawa na 15.2% wakati wastani wa watafitiwa 6.2 (5.4%) hawakujibu kipengee kimojawapo cha msamiati.

Tathmini ya kina inaonesha kuwa ufaulu upo juu zaidi kwenye msamiati wa biashara kwa kuwa na watafitiwa 70 (60.8%) waliofaulu ulinganishwa na 20 (17.4%) waliofeli na 19 (16.5%) ambao hawakujaribu. Ulinganifu wa kijinsia unaonesha utamalaki wa ufaulu kwa wasichana kwani kati ya 70 (60.8%) waliofaulu, 51 (44% ya watafitiwa wote, na 85% ya sampuli ya wasichana) ni wasichana wakati wavulana ni 16.5% ya watafitiwa wote na 34.5% ya wavulana wote ndio waliofaulu. Kwa upande wa msamiati wa ujenzi, waliofaulu kwa ujumla ni 69 (60%) dhidi ya 41(35.6%) waliofeli ambapo miongoni mwao 48 (80%) ni wasichana na 21(38%) ni wavulana. Hivyo wasichana pia wameonesha ufaulu mkubwa katika msamiati wa

ujenzi. Hali ni hivyo hivyo katika msamiati wa kijamii ambapo kati ya watafitiwa 65 waliofaulu, 38 (63.3%) ni wasichana ilihali wavulana walikuwa 27 (49%).

Kulifanyika pia ukokotoaji wa madaraja ya ufaulu wa wanafunzi baina ya wavulana na wasichana katika msamiati na matokeo yake ni kama yanavyoonekana katika kielelezo na 4.4 hapa chini.




**Kielelezo Na. 4.4 : Ufaulu katika Msamiati Kimadaraja**

Kielelezo na.4.3 hapo juu kinaonesha kwamba ufualu umetamalaki zaidi katika msamiati wa kibiashara ambapo wasichana 21(35%) walipata Daraja 'A' na 17 (28.3%) katika Daraja 'B' ingawa hali ni tete kwa wavulana katika masamiati huo (38.2%) walifeli katika Daraja la 'F'. Kwa upande wa msamiati wa kijamii, wavulana 8 (14.5%) na 15 (27.3%) walifaulu katika madaraja ya 'A' na 'B' ingawa bado wasichana walionesha kuwa na uwezo mkubwa kwani 20 (33.3%) na 8 (13.3%) ndio waliopata madaraja hayo. Katika msamiati wa ujenzi utamalaki wa ufaulu kwa wasichana pia ulikuwa bayana kwa kuwa na waliopata madaraja ya 'A'

na ‘B’ kuwa 20 (33.3%) na 7(11.7%) dhidi ya wavulana waliokuwa 11 (20%) na 11(20%) kwa madaraja hayohayo. Kwa ujumla utofauti wa aina ya msamiati haukuweza kuonesha kwamba wenye jinsi ya kike wangeweza kuwa na ufaulu hafifu zaidi ya wanaume ingawa msamiati wa kijamii walionekana kutotamalaki sana.

Tafiti fanani katika wigo huu wa msamiati ni pamoja na ule wa Llach na Gallego (2012) waliotafiti tofauti za kijinsia katika uamiliaji wa msamiati kwa vijana 176 (wavulana 94 na wasichana 82) waliokuwa wanaamili Kiingereza kama lugha ya Kigeni. Utafiti wao ulinesha kuwa, pamoja na mambo mengine, wanafunzi wa kike walionesha umilisi mkubwa zaidi ya wale wa kiume katika msamiati katika hatua tatu za awali ila katika hatua mbili za mwisho, wavulana ndio walionesha kuwapiku wasichana. Utafiti mwingine ni ule wa Boyle (2006) aliyepima umillisi linganifu katika usikilizaji na uelewa wa msamiati kati ya wanaume na wanawake kwa wanafunzi 285 wa Kichina waliokuwa wanaamilia Kiingereza kama lugha ya Kigeni. Walitumia majaribio kumi ya umilisi kama mbinu pekee za kukusanyia data. Matokeo yalionesha kuwa wanafunzi wa kike walionesha umilisi wa juu zaidi katika umilisi wa jumala wa lugha ila wale wa kiume walionesha kuwa na umilisi zaidi katika kusikiliza na kuelewa msamiati.

#### 4.2.2.3 Utambuzi wa Matumizi ya Nafsi katika Tungo

Mtafiti alitumia pia jaribio la umilisi kuwapima wanafunzi watafitiwa uwezo wao wa kutambua matumizi ya nafsi katika tungo. Watafitiwa walielekezwa kutambua kazi ya kipashio kilichopigwa mstari katka tungo anuwai 12 : tungo 3 zilikuwa na njeo za nafsi ya kwanza umoja (*mimi*), 3 nafsi ya kwanza wingi (*sisi*), 3 nafsi ya pili umoja (*wewe*), 3 nafsi ya pili wingi (*ninyi*), 3 nafsi ya tatu umoja (*yeye*) na 3 nafsi ya

tatu wingi (*wao*). Mazingira ya utokeaji wa njeo nafsi hizi ni katika kauli tenda. Matokeo (kwa waliofaulu tu) ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali na. 4.4 hapa chini.

**Jedwali Na.4.4 : Ufaulu katika Viwakilishi Nafsi**


| Nafsi | | Ufaulu | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Ke (n=60) | Me (n=55) | Jumla (n=115) |
| Nafsi ya 1 | Umoja (*mimi*) | 57 | 47 | 104 |
| | Wingi (*sisi)* | 51 | 52 | 103 |
| Nafsi ya 2 | Umoja (*wewe*) | 58 | 49 | 107 |
| | Wingi (*nyinyi*) | 60 | 54 | 114 |
| Nafsi ya 3 | Umoja (*Yeye*) | 57 | 51 | 108 |
| | Wingi (*Wao*) | 60 | 48 | 108 |
| Jumla | | 343 | 301 | 644 |
| Wastani | | 57.2 | 50.2 | 107.3 |

Kwa mujibu wa Jedwali na. 4.4, umilisi wa kiisimu katika kipengele cha viwakilishi nafsi ulikuwa wa juu kwa wengi wa watafitiwa ambapo wastani wa 107.3 (sawa na 93.3%) walifaulu, miongoni mwao wasichana wakiwa ni wastani wa 57.2 (sawa na 95.3% katika kundi lao) na wavulana wakiwa ni wastani wa 50.2 (sawa na 91.2% katika kundi lao). Uchanganuzi wa kina unaonesha ufaulu mkubwa sana katika nafsi ya pili (wingi na umoja) kwa makundi yote ingawa bado wasichana waliongoza kwa wingi wa ufaulu; kwa mfano wote 60 (100%) walifaulu katika nafsi ya pili wingi (kama pia kwa nafsi ya tatu wingi) wakati wavulana walikuwa 48 (87.3%).

Kingine kilicho cha upekee katika data hizi za jedwali na.4.4 ni wavulana kufaulu kwa wingi (52, sawa na 94.5% katika kundi lao) zaidi ya wasichana (50, sawa na 83.3% katika kundi lao) katika umilisi wa viwakilishi nafsi ya 2 wingi. Ingawa

tufauti ni ndogo, bado hii ni mabadliko ya mwelekeo wa utamalaki dhidi ya wasichana ambao walionesha kutamalaki sehemu nyingine za kiisimu ya Kiswahili.

Baada ya kukokotoa ufaulu wa wanafunzi kimadaraja, matokeo kwa ujumla ni kama yanavyoonekana katika kielelezo na.4.5 hapa chini.




**Kielelezo Na. 4.5: Ujumla Linganishi Ufaulu Kimadaraja**

Kadiri ya mtokeo ya ujumla wa umilisi wa viwakilishi nafsi kama yalivyooneshwa kwenye kilelezo na.4.4 hapo juu, wanafunzi walio wengi (jumla yao 74.3, sawa na 64.5% ya watafitiwa wote) walipata ufualu wa Daraja ‘A ‘ likimaanisha wenye umulisi wa hali ya juu katika utambuzi wa viwakilishi nafsi. Miongoni mwa hao, wasichana ndiyo wengi kwani walikuwa wastani wa 42, sawa na 70% ya wasichana wote wakati katika kundi la wavulana walikuwa ni watani wa 32.3, sawa na 58.7%. Katika daraja ‘B’ linalomaanisha umilisi mzuri, wavulana walikuwa na wastani wa wingi zaidi ya wasichana kwani walikuwa ni wastani wa 7.9 (14.4%) dhidi ya ule wa

wasichana, ambao ulikuwa ni 5.4 (9%) pekee. Hata hivyo wavulana, japo kwa uchache wa waliopata madaraja ya chini, wanaonekana ndio wengi kuliko wasichana ikiashiria kuwa wasichana bado walikuwa na umilisi mkubwa zaidi ya wavulana katika viwakilishi nafsi.

Katika kudadavua umilisi wao katika viwakilishi nafsi kimojakimoja, kikokotoo cha excel kilitupa matokeo kama yalivyo kwenye jedwali na.4.5 hapa chini.

**Jedwali Na.4.5: Ufaulu wa Kimadaraja katika Utambuzi wa Nafsi**

| **Viwakilishi Nafsi** | | **Madaraja** | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **A** | | **B** | | **C** | | **D** | |
| | | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** | **KE** | **ME** |
| Viwakilishi Nafsi 1 | Umoja | 37 | 31 | 18 | 10 | 9 | 6 | 7 | 8 |
| | Wingi | 47 | 43 | 3 | 9 | 1 | 0 | 9 | 3 |
| Viwakilishi Nafsi 2 | Umoja | 48 | 31 | 7 | 11 | 3 | 8 | 2 | 6 |
| | Wingi | 54 | 38 | 6 | 9 | 0 | 5 | 0 | 1 |
| Viwakilishi Nafsi 3 | Umoja | 51 | 42 | 1 | 9 | 5 | 0 | 3 | 4 |
| | Wingi | 57 | 41 | 3 | 7 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| **Jumla** | | **294** | **226** | **38** | **55** | **18** | **19** | **21** | **29** |
| **Wastani** | | **42** | **32.3** | **5.4** | **7.9** | **2.6** | **2.7** | **3.0** | **4.1** |

Kwa mujibu wa jedwali na.4.5 hapo juu umilisi kwa wote upo katika daraja la A zaidi kuliko daraja yote na wasichana ndio wenye utamalaki mkubwa zaidi ya wavulana. Hata hivyo, viwakilishi nafsi ya tatu, umoja na wingi, ndivyo vilionesha kuwepo na watafitiwa wengi zaidi kuliko wengine hasa kwa wasichana waliokuwa 51 (85%) kwa upande wa umoja na 57 (95%) kwa upande wa wingi ili hali walivulana walikuwa 42(76.4%) na 41 (74.4%). Kwa upande wa viwakilishi nafsi ya pili, wasichana pia walifanya vizuri sana hasa kwenye wingi ambapo 54 (90%)

walipata daraja ‘A’ ilihali wavulana waliofaulu katika daraja hilo kwa nafasi ya pili wingi walikuwa 38 (69%). Nafsi ya kwanza (wingi na umoja) japo bado kulionesha kwamba wengi wa watafitiwa katika makundi yote mawili walipata Daraja ‘A’, hao hawakuwa wengi wakilinganishwa na nafsi ya pili na ya tatu.

Kwa ujumla umilisi wa kiisimu katika viwakilishi nafsi ulikuwa wa hali ya juu, huku wasichana wakifanya vizuri zaidi kuliko wavulana.

Kumefanyika pia tafiti tangulizi yenye mfanano na huu katika umilisi wa kisintaksia. Kwa mfano, utafiti wa Tse na wenzie (2002) ulijikita katika tofauti kati ya watoto wa kike na wa kiume katika uamiliaji wa sintakisia ya Kiingereza. Walichambua senstensi za watoto wenye umri katika ya miaka mitatu hadi mitano. Mtokeo ya uchambuzi wao yalionesha kuwa watoto wa kike walifanya vizuri zaidi ya wale wa kiume katika wastani wa urefu wa sentensi na aina za sentensi.

Halikadhalika, utafiti wa Signell (2012) kwa watoto wa Kiswidi waliokuwa wanaamilia Kiingereza kama lugha ya kigeni, aling’amua kuwa kulikuwa na ombi la kijinsia katika uamiliaji huo ambapo kwa wanafunzi wa madarasa ya kati na yale ya juu wanafunzi wa kike walifanya vizuri zaidi kuliko wale wa kiume katika umilisi wa kisintaksia.

## 4.3 Vichocheo na Vipingamizi vya Umilisi Uliobainika

Sehemu hii  inajibu lengo mahususi la pili lililolenga kutathmini kichocheo au kipingamizi cha umilisi uliobainika katika lengo mahususi namba 1. Swali mahususi la pili nalo lilihoji: *Ni  nini kichocheo au kipingamizi cha ubobezi uliobainika katika lengo na. 1 hapo juu* ?

Mtafiti alitumia maswali ya dodoso yaliyolenga kujua sababu zinazochangia watafitiwa kuwa na tofauti za umilisi baina ya wavulana na wasichana katika lugha ya Kiswahili. Dodoso liligawanyika katika sehemu kuu tatu : a) mbinu za kujifunzia, b) tathmini ya ufundishaji na utoshelevu wa vifaa vya kujifunzia na 3) utayari wa kuwasiliana kwa Kiswahili.

### 4.3.1 Mbinu za kujifunza kama Kichocheo au Kikwamizo

Kwa njia ya dodoso lililoweka vipengee kadhaa toka kwenye dodoso asili la Oxford (1990) lihusulo mbinu za kujifunzia, wanafunzi walijibu kwa kwa kadiri ya makundi yao kama jedwali na.4.6 linavyoonesha. Lengo lilikuwa kubaini mbinu za ujifunzaji kama kichocheo au kikwazo cha fanaka katika umilisi isimu kama kilivyopimwa hapo juu (sehemu 4.2). Matokeo yake ni kama yanavyoonekana kenye jedwali 4.6 hapa chini.

**Jedwali Na. 4.6: Majibu Kuhusu Mbinu za Ujifunzaji**

| s/n | Mbinu za kujifunzia | natumia | | siitumii | | Sina hakika | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KE | ME | KE | ME | KE | ME |
| 1 | Kukariri yanayofundishwa darasani | 13 | 38 | 40 | 15 | 7 | 2 |
| 2 | Kusoma zaidi vitabu vya isimu ya Kiswahili | 46 | 21 | 11 | 27 | 3 | 7 |
| 3 | Kujisomea zaidi ya darasani | 42 | 46 | 9 | 8 | 9 | 1 |
| 4 | Ubunifu katika kuitumia lugha | 48 | 11 | 10 | 29 | 2 | 15 |
| 5 | Kuulizauliza maana ya mambo yahusuyo sarufi na msamiati | 53 | 8 | 5 | 24 | 2 | 23 |
| 6 | Kuandika zaidi ninaposikiliza | 41 | 36 | 14 | 11 | 5 | 8 |
| 7 | Kufurahia tamthiliya na nyimbo za Kiswahili | 54 | 22 | 6 | 18 | 0 | 15 |

Kadiri ya matokeo kwenye jedwali na. 4.6 hapo juu, udadisi kwa maana ya kupenda kuulizauliza mambo yahusuyo sarufi na msamiati na kufurahia tamthiliya na

nyimbo za Kiswahili ni mbinu wasichana walio wengi (53, sawa na 88.3% na 54, sawa na 90%) ukilinganisha na wavulana (8, sawa na 15.5% na 22, sawa na 40%) katika kujifunza Kiswahili. Udadisi wa mambo na kupenda kusikiliza lugha ikitumiwa hukuza na kupanua uelewa na msingi ya kiisimu ya lugha husika kwa wajifunzaji, na hili ni ashirio bayana kwa nini wasichana walionekana kuwa na umilisi mkubwa kuliko wavulana katika vipengele anuwai vya lugha ya Kiswahili. Hali kadhalika wasichana walio wengi wameonesha kutumia mbinu za kusoma zaidi vitabu vya isimu (46, sawa na 76.6%, dhidi ya wavulana 21, sawa na 38.2%), kupenda ubunifu katika kutumia lugha (48, sawa na 80%, dhidi ya wavulana 11, sawa na 20%) na kuandika zaidi wakati wakisikiliza (41, sawa na 68.3% dhidi ya wavulana 36, sawa na 65.4%). Sababu hizi huwa ni kichochea cha umilisi wa kiisimu hasa kufahamu isimu kwa kughamua zaidi wakati muamiliaji anapoitumia lugha lengwa, zaidi ya kufundishwa tu darasani. Hili pia limeonesha kwa nini wasichan wengi zaidi ya wavulana walionesha umilisi wa isimu ya Kiswahili katika vipengee walivyopimwa. Hali ni tofauti katika kutegemea na kukariri yaliyofundishwa dara sani pekee ambapo wavulana walio wengi 38, sawa na 69%, dhidi ya wasichana 13, sawa na 21.7%) walionesha kuitumia mbinu hii. Utegemezi na ukariri wa sheria na kanuni za lugha huwa na matokeo hasi ya kiumilisi wa lugha na hivyo huwa kama kikwazo cha ufanisi wa uamiliaji isimu ya lugha. Hii huenda pia ikaakisi kwa nini wavulana walio wengi hawakuonesha umilisi wa kutosha kwenye matokeo ya upimaji.


Utafiti fanani katika hili ni ule wa Burman (1993), aliyetaka kuathmini utofauti wa mbinu za kujifunza lugha baina ya wavulana na wasichana. Aligundua kwamba

wavulana walipendelea zaidi kukariri maneno na sentensi kwa msaada wa picha zilizochorwa. Pia utafiti wa Wang (2004) aliyetafiti mbinu za kujifunzia za wanafunzi 59 wa shada za awali wa Kichina, aligundua kuwa wengi wa anaume walipendelea zaidi kujifunza kwa njia za kukariri maneno/ msamiati.

Kwa ujumla, mbinu za ujifunzaji, zimeonesha kuwa wasichana walitumia zaidi mbinu zile zinazochochea ufanisi wa umilisi lugha kuliko wavulana. Kwa mantiki hiyo, kumekuwa na uhusiano chanya kati ya mbinu za kujifunzia na kiwango cha umilisi lugha kwa watafitiwa wa utafiti huu.

### 4.3.2 Tathmini ya Ufundishaji na Utoshelevu wa Vifaa vya Kufundishia

Kipengee cha pili kilicholengwa kuchunguza vichocheo au vikwamizaji vya umilisi wa lugha kwa matokeo ya umilisi wa lengo la kwanza la utafiti kilihusiana na wanafunzi wanavyoona na kutathmini mbinu za ufundishaji na mazingira ya kipedagojia. Matokeo ya ujazaji dodoso katika kipengee hiki ni kama yanavyoonekana kwenye kielelezo na.4.6 hapa chini.




**Kielelezo Na. 4.6: Maoni Kuhusu Mbinu za Ufundishaji na Utoshelevu wa Vifaa vya Kufundishia**

Matokeo ya dodoso kuhusu nafasi ya mbinu za kufundishia yanaonesha wasichana wengi (54, sawa na 90%) zaidi kuliko wavulana (45, sawa na 81.Kuhusu haiba ya mwalimu kuwa ya kuvutia kuelewa vizuri, pia nusu (30, sawa na 50%) ya wasichana walikubaliana na hili dhidi ya wavulana 21(38.1%) ambao walikubaliana huku wengine 27 (49%) wakikataa hilo. Hata hivyo, kuhusu urahisi au wepesi wa kuelewa kwa sababu ya lugha anayoyumia mwalimu, ni wavulana waliokuwa wengi (41, sawa na 74.5%) zaidi ya wasichana (24, sawa na 40%) kukubaliana na kipengee hicho. Kwa ujumla, vyote hivyo ni vichocheo vya ufanisi wa umilisi lugha katika muktadha wa darasani na makundi yote yalionesha kukubaliana japo ni wasichana waliozidi wavulana isipokuwa wepesi wa lugha ya waalimu wao.

Kipengele ambacho makundi yote yalikiona kuwa ni kikwamizo katika umilisi wa isimu ya Kiswahili ni utoshelevu wa vitabu vya kufundishia ambao wengi sana katika makundi yote mawili walionesha kutokukubaliana. Katika kipengee hiki


wasichana 57 (95%) na wavulana 52 (94.2%) hawakukubalina na kauli ya utoshelevu wa vitabu. Kwa mantiki hii, hapakuwa na tofauti kati ya jinsia zote kuhusu vifaa vya kufundishia kutotosheleza.

Watafiti Murphy & Elwood (1998) wanashadidia kuwa wavulana huwa na hamasa zaidi kuliko wasichana katika mambo ya ujifunzaji lugha kwenye mazingira ya darasani. PiaVan der Silk na wenzake (2015) wana maoni kwamba tafiti nyingi zimefanyika kuonesha kuwa wasichana huwa na hamasa kubwa zaidi katika ujifunzaji wa lugha kuliko wavulana. Maoni haya yanalandana na data katika kipengele hiki cha kichocheo au kikwamizi cha fanaka katika umilisi wa isimu ya lugha. Hii ni kwa vile maoni ya wasichana yaliowapiku wavulana katika nafasi ya mambo kadhaa ya kidarasani kama vichocheo vya ufanisi wa umilisi lugha ya Kiswahili.

Zipo pia tafiti fanani katika kipengele hiki. Mojawapo ni utafiti wa Diab (2000) ulichunguza mbinu za kujifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili kwa wanafunzi 284 (wasichnana 57% na wavulana 43%) katika vyuo vikuu vitatu vya Kilebanoni. Waligundua uwepo wa tofauti kubwa ya kijinsia kati ya namna ya ujifunzaji wa lugha huku wanafunzi wa kike wakionesha kutumia mbinu anuwai za kujifunza lugha kuliko wanaume.

### 4.3.3 Utayari wa Kuwasiliana kwa Kiswahili

Utayari wa kuwasiliana kwa kutumia lugha lengwa (Kiswahili) kilikuwa kipengele cha tatu cha dodoso katika kudadavua vichocheo au vikwamizo vya umilisi wa kiisimu. Watafitiwa walijibu kipengee hiki tofauti tofauti kama kielelezo na.4.7 kinavyotanabaisha.




**Kielelezo Na. 4.7: Maoni kuhusu Nafasi ya Mbinu za Kujifunza Lugha**

Kadiri ya kielelezo na. 4.7 hapo juu, kulikuwa na kauli nne ambapo wanafunzi watafitiwa waliombwa kuonesha kukubaliana au la. Katika kipengee cha kupenda kuwasiliana kwa Kiswahili nje ya darasa, wasichana wengi (54, sawa na 90%) kuliko wavulana (40, sawa na 72.7%) walikubaliana kuwa wanapenda hilo. Wasichana walitamalaki kiidadi (45, sawa na 75%) dhidi ya wavulana 21, sawa na 38%) na pia katika vipengee vya kupenda kuwasiliana wakiwa nyumbani kwa Kiswahili na katika kutamani wangefundishwa masomo yote kwa Kiswahili (58, sawa na 96.5%) dhidi ya wavulana 45, ambao ni sawa na 81%).

Hata hivyo wavulana walitamaki kiidadi (41, sawa na 74.5%) dhidi ya wasichana (20, sawa na 33.3%) katika kukubali kuwa walikuwa wanawasiliana kwa Kiswahili pale tu mwalimu anapokuwepo. Kauli hii inaashiria kikwazo cha ufanisi wa umilisi na ni kiashirio cha kwa nini pia wavulana walio wengi hawakuwa na umilisi wa juu wa isimu ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Wright (1999), wasichana wana mtazamo chanya zaidi ya wavulana kwenye uhiyari wa kuwasiliana kwenye lugha wanayoiamili. Nao utafiti wa Sinnett na Alishah (2021) ulihusisha wanafunzi 119 wa kiume na 163 wa Kituruki waliokuwa wanasoma Shahada za awali katika vyuo vikuu vya Uturuki. Lengo lao lilikuwa kufanya tathmini linganifu baina ya wanaume na wanawake katika uhiyari wa kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza. Waling'amua kuwa tofauti ni ndogo baina ya makundi haya mawaili ingawa wanawake walionesha utayari wa kuwasiliana zaidi ya wanaume katika miktadha anuwai.

Vilevile utafiti wa Valadi na wenzake (2015) uliotafiti nafasi ya jinsia kama kitofautishi cha uhiyari wa kuwasiliana kwa wanafunzi 140 wa Irani waliokuwa wanajifunza Kiingereza kama lugha ya kigeni haukuona tofauti kubwa baina ya wanaume ana wanawake. Hata hivyo, utafiti wa Altıner (2018) uliohusha wanafunzi 711 waliokuwa wanajifunza Kiingererza kama lugha ya kigeni huko Chuo Kikuu cha Uturuki ulibainisha kuwa wanafunzi wa kike walikuwa na uhiyari mkubwa zaidi wa kuwasiliana kuliko wale wa kiume.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazo zilipatikana kwa kutumia mbinu ya jaribio la umilisi na hojaji. Uwasilishaji wa uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti huu na umeongozwa na mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi. Aidha, Nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981) ilitumika katika uchambuzi wa data. Matokeo yameonesha kuwa wasichana ndiyo wenye umilisi mkubwa wa kiisimu ukilinganisha na wavulana, matokeo ambayo tafiti fanani pia zilionesha.

Sura inayofuata baada ya sura hii, inawasilisha muhutasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu kuhusu upimaji wa ufahamu wa Kiswahili katika shule za sekondari. Sehemu ya kwanza ya sura hii inahusu muhtsari, sehemu ya pili ni hitimisho na sehemu ya tatu ni mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

### 5.2.1 Muhtasari wa Jumla

Utafiti huu ulikusudia kutathmini umilisi wa isimu ya Kiswahili kama lugha ya pili kwa kulinganisha wasichana na wavulana wa shule za sekondari Tanzania kutumia mfano toka wilaya ya Mufindi. Ili kufanikisha lengo kuu, utafiti ulikuwa na madhumuni mahsusi mawili ambayo ni kupima utofauti au mfanano wa umilisi wa isimu ya Kiswahili kama lugha ya pili baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume wa shule za sekondari na pili, kutathmini kichocheo au kikwamizi cha utofauti au mfanano wa kijinsia wa kiumilisi uliobainika katika lengo na. 1 hapo juu. Utafiti huu ulijikita katika nyanja za kiisimu hususan aina za maneno, msamiati, na viwakilishi nafsi na ulihusu wanafunzi wa shuke za sekondari pekee. Utafiti uliongozwa na nadharia ya umilisi wa mawasiliano ya Canale na Swain (1980, 1981) ila ulijihusisha na kipengere kimoja tu, ambacho ni umilisi wa isimu. Utafiti huu pia ulikuwa wa kifani kwa upande wa usanifu na mchanganyiko wa kiidadi na kimaelezo kwa upande wa mkabala. Katika utafiti huu watafitiwa 115 (wavulana 55 na wasichana 60) waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu. Mbinu mbili zilitumika kupata data ambazo ni jaribio la umilisi na hojaji.

### 5.2.2 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu wanafunzi walipimwa juu ya umilisi walionao katika isimu ya lugha ya Kiswahili.

Katika lengo la kwanza la utafiti, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa wasichana wametamalaki kwa wingi katika njanja zote za isimu zilizopimwa, kama ifuatavyo:

- katika tathmini binafsi ya umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili, zaidi ya theluthi mbili za wasichana walijiona wanao umilisi wa juu wa kiisimu wakati ni wavulana theluthi moja tu ndiyo wajiona kuwa na umilisi huo.

- Katika kutambua na kubaini aina za maneno, wasichana karibia robo tatu walifauli katika vivumishi dhidi ya wavulana ambao idadi yao ilikuwa wastani wa nusu. Hii ilifuatiwa na vielezi ambapo pia wasichana waliongoza kwani nusu yao walifaulu wakati wavulana walikuwa chini ya robo. Vitenzi vilikuwa na ufaulu hafifu kwa makundi yote kwa kuwa na wasichana chini ya theluthi moja na wavulana chini ya asilimia ishirini tu waliofaulu.

- Katika matumizi ya msamiati, ufaulu ulikuwa juu zaidi kwenye msamiati wa biashara na ulinganifu wa kijinsia unaonesha utamalaki wa ufaulu kwa wasichana kwani kati ya zaidi ya theluthi mbili walifaulu wakati wavulana ni chini ya asilimia ishirini ndio waliofaulu. Kwa upande wa msamiati wa ujenzi, wasichina asilimia themanini walifaulu dhidi ya wavulana ambao ufualu wao ulikuwa wastani wa theluthi moja.

- Katika matumizi ya viwakilishi nafsi, ufaulu ulikuwa wa juu kwa wengi wa watafitiwa ambapo wastani wa takribani asilimia tisini walifaulu, miongoni

mwao wasichana wakiwa ni asilimia tisini na tano katika kundi lao ilihali na wavulana walikuwa asilima tisini na moja katika kundi lao.

Hata hivyo, wavulana walitamalaki katika umilisi wa viwakilishi nafsi ya 2 kwani walikuwa ni wastani wa zaidi ya asilimia tisini katika kundi lao wakati wasichana walikuwa wastani wa asilimia themanini na tatu katika kundi lao.

Kwa upande wa lengo la pili la utafiti lililolenga kutambua vichocheo au vikwamizi vya umilisi:

- wasichana bado walionesha utamalaki katika vichocheo vya umilisi katika nyanja za mbinu za kujifunza lugha ilihali wengi wa wavulana walionesha kukariri na kutegemea vitini vya mwalimu kama mbinu ya kujifunzia (ambacho ni kikwamizi).

- Katika maoni kuhusu mbinu za kufundishia kama vichocheo vya ufanisi wa umilisi makundi yote yalionesha kukubaliana japo ni wasichana waliozidi wavulana isipokuwa katika wepesi wa lugha ya waalimu wao kama kichocheo ambapo wavulana ndio waliokuwa wengi.

- Kwa upande wa uhiyari wa kuwasiliana, wasichana walitamalaki kiidadi katika vipengee vya kupenda kuwasiliana wakiwa nyumbani kwa Kiswahili na katika kutamani wangefundishwa masomo yote kwa Kiswahili.

- Hata hivyo wavulana walitamaki kiidadi dhidi ya wasichana katika kukubali kuwa walikuwa wanawasiliana kwa Kiswahili pale tu mwalimu anapokuwepo.

## 5.3 Hitimisho

Kwa mantiki ya matokeo hapo juu, inaweza kuhitimishwa kwamba :

- Jinsia ni kisababishi kikubwa katika utofauti wa umilisi walionao wanafunzi katika nyanja za kiisimu. Hii ni kwa vile utamalaki haukufanana kwa ulinganifu wa kiisimu.

- Wasichana au waamiliaji lugha wa jinsia ya kike wana umilisi mkubwa kuliko wavulana au wanaume katika nyanja nyingi za kiisimu. Hii imejidhihirisha sana katika data zilizopatikana katika utafiti huu.

- Upo uhusiano chanya na wa nguvu katika ya mbinu za kujifunzia lugha, mbinu za kufundishia na uhiyari wa kuwasiliana, kwa upande mmoja, na kiwango cha umilisi cha upande mwingine. Waliochagua zaidi vichocheo katika njanja waliazoulizwa kwenye hojaji (na ambao ni wasichana) ndio hao pia walionesha umilisi mkubwa kuliko waliochagua vikwamizi (ambao wengi wao walikuwa wavulana).

## 5.4 Mapendekezo

### 5.4.1 Mapendekezo ya Jumla

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kwamba serikali ione uwezekano wa kulipa kipaumbele suala la uboreshaji wa ufundishaji wa somo la Kiswahili na hasa kipengee cha isimu. Pia upatikanaji wa vitabu na zana nzuri na toshelevu za kufundishia iwe sehemu ya vipaumbele vya ufanisi katika ufundishaji somo la Kiswahili. Tatu, hamu kubwa waliyoonesha watafitiwa ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kutathminia masomo mengine katika ngazi ya sekondari iwe

chachu kwa serekali kuibua upya majadala wa lugha ya Kiswahili kuwa lugha mwenza, sambamba na Kiswahili, kama lugha ya kufundshia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti huu ulijikita katika tathmini linganifu ya umilisi wa isimu ya Kiswahili kama lugha ya pili. Tunapendekeza utafiti fuatishi utakaolenga kulinganisha nyanja nyingine za wajifunzaji kama vile umri, mahali lugha tangulizi na haiba za wanafunzi kama vigezo vya utafiti katika ufanisi wa umilisi.

Pili, mtafiti hakuvifanyia kazi vipengee vyote vya kiismu katika mtaala wa elimu ya sekondari kama vile umilisi katika utumizi katika lugha za kisanii, ufahamu na ufasaha wa usomaji. Mapendekezo ya mtafiti ni kwamba tafiti zingine zinaweza kufanyika juu ya nyanja hizo pia.

Tatu, utafiti mwingine linganifu wa upimaji wa umilisi ufanyike katika nyanja za kulinganisha uhusiano uliopo baina ya umilisi katika lugha ya mazungumzo na umilisi katika lugha mfumo katika lugha ya Kiswahili.

**MAREJELEO**

Adam, J. na Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies*, Morogoro: Mzumbe Book Project.

Alahmadi, N.S. & Lahlali, M. (2019). The Role of Learners’ Gender Differences in L2 “Inter-Language” Errors of Intermediate- Level Saudi Language Learners. *Journal of Arts and Humanities*, 8(10), 63-74.

Altıner, C. (2018). Turkish EFL learners' willingness to communicate in English. *International Journal of Contemporary Educational Research* 5(1), 40-49

Babyegeya, E. (1998). *Test and Measument*. Dar es Salaam: Open University of Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.

Bachman, L. F na Palmer, A.S (1996). *Language Testing in Practice*. Buck: Oxford University Press.

Bhaiji, A. F. (1976). The Medium of Instruction in Our Secondary Schools. A Study Report in Education and Devolopment. Department of Education, University of Dar es Salaam. Dar es Salaam, Tanzania

Boyle, J. P. (1987). Sex differences in Listening Vocabulary. *Language Learning*, 37(2), 273-284.

Brock-Utne B., Desai, Z. and Qorro, M.A.S. (2005). *LOITASA Research in Progress. Language of Instruction in Tanzania and South Africa*.Dar es Salaam: KAD Associates.

Brock-Utne, B. (2000). *Whose Education for All? Re-colonization of the African Mind*. New York: Falmer press.

Brock-Utne, B. (2003). Language Question in Africa in the Light of Globalisation, Social Justice and Democracy. *International Journal of peace studies*, vol. 8 uk 2

Brock-Utne, B. (2006). *The Continued Battle over Kiswahili as the Language of Instruction inTanzania.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota

Brock-Utne, Desai Z.and Qorro, M.A.S. (eds), (2003). *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA).*Dar es Salaam: E& D publishers

Burman, D. D. (1993*). Gender differences in language abilities evidence from brain imaging*. New York: Cassell.

Canale M. na Swain M.(1980). Theoratical base of Communication Approach to Second language teaching and testin *applied linguistics*, Vol. 1, pp. 1-47.

Canale, M. & Merrill S. (1980). "Theoretical base of communicative approaches to second Language teaching and testing", *International journal for applied linguistics*

Canale, M. (1983). "From Communicative Competence to Communicative Language Pedagogy" In: Richards J, Schmidt R (eds). *Language and Communication*. London: Longman.

Canale, M. na M. Swain (1980). *Theoretical Bases of Communicative Approaches to Second Language Teaching and Testing. Applied Linguistics*. London: Longman.

Carell, D (1993). *Metacognitive Strategy Training for ESL Reading*, USA: Wiley Browse pub, Ltd

Chimera, R. (1998). *Kiswahili Past, Present and Future Horizons*, Nairobi: OUP

Chiragdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: O.U.P.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax.* Cambridge: Mass MIT press.

Chomsky, N. (1976). *Reflections on Language.* London: Temple Smith.

Chomsky, N. (1986). *Knowledge of language, its nature and use*. Cambridge: Mass MIT Press

Chomsky. N. (1957). *Syntactic Structure Cambridge:* Cambridge University press.

Coseriu, E. (1985). *Linguistic competence: what is really? The modern language Review*. Cambridge: Cambridge university press.

Criper, C. & Dodd, W. (1984). *Report on the Teaching of English Language and its Use as a Medium of Education in Tanzania.* The British Council. Dar es Salaam, Tanzania.

Crystal D. (1997). *The Cambridge Encyclepedia of language*. London: Cambridge university press

Desai, C. and Qorro, M.A.S. (eds) (2003). *The language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA*).Dar es Salaam: E&D Publishers.

Diab R. (2000). Political and socio-cultural factors in foreign language education: The Case of Lebanon. *Texas Papers in Foreign Language Education* 5, 177-187.

Ellis, R. (1994). *The study of Second Language Acquisition*. London: Oxford University Press

Enon, C. J. (1998). *Education Research and Measurement*, Department of Distance Education, Makerere University, Uganda.

Essa, R. (2001). Evaluation of oral efficiency of intermediate school teachers of English. Unpublished MA Thesis, University of Al Mustansiriyah, college of Teachers.

Fillmore & Charles, J. (1979). *Individual differences in language ability and language Behavior. New York*: Academic press

Główka, D. (2014). The impact of gender on attainment in learning English as a foreign language, *Studies in Second Language Learning and Teaching*. SSLLT 4 (4). 2014. 617-635 doi: 10.14746/ssllt.2014.4.4.3

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*.Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Halliday, M. A. K. (1973). *Exploration in the Function of Language.* London: Edward Arnold.

Heine, B. (1992). “Language Policies in Africa”. In: R. Herbert (ed.), *Language and Society in Africa. The Theory and Practice of Sociolinguistics*, pp. 23–35. Cape Town: Witwatersrand University Press.

Hymes, H. (1971). *Competence and performance in Linguistic theory language acquisition. Models and Methods.* London & New York: Academic Press.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2011).*Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi: Sera ya Elimu na Mafunzo 2010*. Dar-es Salaam, Tanzania.

Jokey, M. (2007). An assessment of intermediate school Teachers English classroom, Unpulished MA. Thesis. University of Baghdad

Kamau, M, (2015). Taathira za Kiswahili na lugha nyingine kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama: Mfano wa lugha ya Kikuyu. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kamugisha, D. J. na Mateng’e, F.J. (2004). Politics of Curriculum Making: A Quandary to Quality Education in Tanzania? *International Journal of social science and Enterpreurship* 1pg 9.

Kaplan, R. na Baldauf, R. (1997). *Language Planning from Practice to Theory*. Clevedon: Multiligual matters

Kombo, D. and D. Tromp (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publication Africa.

Kothari R. (2012**).** Research Methodology: Methods and Techniques (Second Revised Edition). New Delhi: New age International Publishers.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology Methods and Technique (Second Revised Edition).* New Delhi: New age International Publishers.

Kothari, R. C. (1990). *Reseach Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi. New Age International (P) Limited.

Kothari, R. C. (2008). *Research Methodology; Methods*. New Delhi New Age International Publishing LTD.

Koul L. (2009). *Methodology of Educational Research*, fourth Revised and Enlarge Edition. Inda Vikas publishing House PVT Ltd: New Delhi India.

Koul, O. N. (2008). Modern Hindi grammar. S*pringfield*, VA 22150, USA: McNeil Technologies, Inc. http://www.iils.org/pdf/ModernHinduGrammar.pdf

Krashen, S. D. na Tracy D. T. (1983), *The Natural Aproach Language Acquisition in The Classroom*. Oxford: Pergamon Press.

Lehmann, C. (2006). Linguistic competence. Erfurt. University of Erfurt publ

Llach, M.P, & Gallego, M.T. (2012). Vocabulary Knowledge Development and Gender Differences in a Second Language. *ELIA* 12, 45-75.

Massamba D. (1989). "An Assessment of the Development and Modernization of Kiswahili Language in Tanzania". In F. Coulmas (Ed) *Language Adaptation*. London: Cambridge University Press.

Massamba, D. Kihore, Y. & Hokororo, J. (2009). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA); Sekondari na Vyuo*, Dar –es –Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

McNamara, T. (2000). *Language Testing*. Hong Kong: Oxford University Press.

Mekacha, R**. (**2000). Isimu jamii-Nadharia na muktadha wa Kiswahili. Minoocity: Osaka university of Foreign studies.

Mekacha, R. D. K. (1997). Language as a Determinant of the Quality of Education.A

Rejoider, *Journal of Linguistics and Language in Education* Vol 3:95-105.

Mekacha.R.D.K. (1995). Kwa nini Kiingereza Bado ni Lugha ya Kufundishia Elimu ya Juu Tanzania? *Kioo cha Lugha, Journal of the Institute of Kiswahili studies, University of Dar es salam.*

Mlama, P. & Matteru, B. (1978). *Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia katika Elimu ya juu.* Dar es Salaam: BAKITA.

Mlama, P. na Matteru, M. (1980). Haja ya kutumia Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia katika Elimu ya Juu. *Lugha Yetu, juzuu ya* 35 na juzuu ya 36.

Mligo, S.E (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki*. Dar es Salaam. Ecumenical Gathering (EGYS).

Mochiwa, Z. S. M. (1979).The Impact of Kiswahili on Ethnic Languages.A Case Study of Handeni District.Unplished M.A. Thesis: University of Dar es Salaam.

Msanjila Y. P. (2009). Haja ya Kuwa na Sera Toshelevu ya Lugha Tanzania: Uzoefu Na Changamoto. *Mulika* Juzuu. 28, kur. 62-71.

Msanjila, P. Y na wenzake (2009). *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam.TUKI.

Msanjila, P. Y na wenzake (2011). *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam. TUKI.

Msanjila, Y. P. (2007). Utumiaji WA Kiswahili Na Lugha za Jamii. Kijinsia nchini Tanzania. *Nordic Journal of African Studies*, Vol.3, No.6, pp. 34-51.

Msanjila, Y.P. (2004). “Kiswahili kitumike kufundishia shule za sekondari na Elimu ya juu Tanzania”.In:Y.M Kihore and A.R. Chuwa (eds.), *Kiswahili katika karne ya Ishirini na moja*. Dar es Salam.TUKI:Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Kurasa 40 –49.

Msanjla, Y. P. (1998). Uzoefu wa kutumia Kiswahili kama Lugha ya kufundishia katika Vyuo vya Ualimu nchini Tanzania. *Journal of Linguistics and Language in Education*, Vol.3, pp 75-95.

Murphy, P & Elwood, J. (1998). “Gendered learning outside and inside school: influences on achievement”. In Epstein, D, Elwood, J, Hey & Maw, J (eds.), *Failings boys? Issues in gender and achievement,* 162-181. Buckingham: Open University Press.

Newmark, P. (1966). How to Interfere with Language Learning*, Internatonal Journal of American Linguistics* 40

Ng’ong’a, O (2002). An assessment of University English language teacher Education in the light of classroom needs.Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa: Maseno niversity.

Nunan, D. (2003). *Practical English Language Teaching*. Singapore: McGraw-Hill Education (Asia)

O-saki, K. M. (2003). Evaluation of Lead Teacher Training Institutes in Ethiopia. A Consultancy Report Prepared for UNESCO. Paris: UNESCO

Peterson, R. (2006). *The use of an African Language as Language of Instruction at University level.The Example of Kiswahili Department at the University of Dar es Salaam in Tanzania*.Oslo: Institute of Educational Research.

Pons, V. (1992). *Introduction to Social Research.* Dar-es-salaam: Dar-es-salaam University Press.

Prah, K. K. (2003). “Going Native: Language of Instruction for Education, Development and African Emancipation”. In B. Brock Utne, Z Depai and Qorro. (Eds). *Languages of instruction in Tanzania.* Dar-es Salaam: E & D Limited.

Puja, G. K. (2003).Kiswahili and Higher Education in Tanzania. Reflections Based

on a sociological study from three Tanzanian university Campuses". In Brock-Utne, Birgit, Zubeida Desai and Martha Qorro (eds), *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E& D publishers

Qorro M. A. S. (2006). Does Language of Instruction Affect Quality of Education? University of Dar es Salaam, Haki Elimu working Papers.Dar es Salaam

Qorro, M. A. S. (2005**). "**Parents' Views on the Medium of Instructions in post-Primary Education in Tanzania". In: B.Brock-Utne, Desai Z. and Qorro, M.A.S. (eds) *LOITASA Research in progress*. Dar es Salaam. KAD Associates.

Ramadhan. K. (1998). Assessing the proficiency competence of primary school teachers of English in Baghdad. Unpublished. MA. Thesis. University of Baghdad.

Richard J.C na Rodgers T.S (2001). *Approaches and Methods in Language Teaching*. New York: Cambridge University press.

Richard, C & Rodgers, S (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching*:. USA, CUP

Rocha, M.C (2011). *Kiswahili Past Present and Future Horizoni,* Nairobi University Press

Rubagumya, C. M. (1991). "Language promotion for educational purposes: the example of Tanzania", in Legère, K. (ed.), *The role of language in literacy programmes with special reference to Kiswahili in eastern Africa.* Bonn: Deutsche Stiftung für Internationale Entwicklung, 198-215.

Rubagumya, C.M (2003). "English Medium Primary Schools in Tanzania. A new Linguistic Market in Educatio*n?"* In: Birgit Brock-Utne, Zubeida, D. and Qorro, M.A.S. (eds), *Language of Instruction in Tanzania and South Africa*.Dar es Salaam: E&D Limited.

Rubanza , Y. I (2013). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuudo*, Dar es salam: Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania.

Rubin, J. & Jenudd, B. H. (Eds) (1971). *Can Language be Planned? Sociolingustic Theory and Practice for Developing Nations*. Honululu: Honululu University Press.

Rudzinska, L. (2013). Are Females Better than Males in Communication in Second Language? *Journal of Education Culture and Society*, (2): 148-154.

Sengo Y. (1995). Hali ya kutatanisha ya Kiswahili hivi leo "Afrika Mashariki" ; makala kwa ajili ya kongamano la nane la Kiswahili chuo kikuu cha Bayreath. tarehe 26 na 27 Mei 1995

Sengo, T.S.Y. (1987) Towards Maturity in Kiswahili Scholarship. *Kiswahili Juzuu* 54, kur 215-224

Senkoro, F. (2004). "The Role of Language in Education and Poverty Alleviation: Tool for Access and Empowerment", in Galabawa J. and Narman, A. (Eds.). *Education Poverty and Inequality* Dar es Salaam: KAD Associates

Signell, K. (2012). Syntactic development in learner English: A T-unit based syntactic analysis of written production by Swedish L2 learners of English. C-paper. Uppsala University: Department of English.

Sinnett, T.J. & Alisha, A.R. (2021). The Effects of Gender on Willingness to Communicate Among Turkish EFL Learners. *European Journal of English Language Teaching*, 6(4), 17-33.

Sökmen, A. J. (1993). 'Word association results: a window to the lexicons of ESL students', *JALT Journal*, 15, 2, 135–150.

Stern, H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching*. Oxford; Oxford University Press.

Stern, H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching*: Oxford; Oxford University Press/

Taasisi ya elimu Tanzania (2005). *Mwongozo wa Tathimini na Upimaji*, Dar-es Salaam, Tanzania.

Taasisi ya elimu Tanzania (2006). *Mwongozo wa Tathimini na Upimaji*. Dar-es Salaam, Tanzania.

Tikolo, O. (2012). English Language In competency amongst senior secondary school Graduates in Nigeria A-801: Education policy Analysis and Research utilization in comparative perspective, Harvard Graduate School of Education, December 12,201.

Trudgill, P. (1983). *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. London: Penguin Book Ltd.

Tse, S., Kwong, S., Chan, C., & Li, H. (2002). Sex differences in syntactic development: Evidence from Cantonese-speaking preschoolers in Hong Kong. *International Journal of Behavioral Development*, 26(6), 509-517. doi: 10.1080/01650250143000463

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2010). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press Vuzo.

UNESCO, (1953). *The Use of Vernacular Languges in Education*, Paris: UNESCO.

Valadi, A., Rezaee, A., & Kogani Baharvand, P. (2015). The relationship between language learners' willingness to communicate and their oral language proficiency with regard to gender differences. *International Journal of Applied Linguistics and English Literature*, 4(5), 147-153. doi: 10.7575/ aiac. ijalel.v. 4n.5p.147

Van der Silk, F.W.P, van Hout, R.W.N & Schepens, J.J. (2015). The gender gap in second language acquisition: Gender differences in the acquisition of Dutch among immigrants from 88 countries with 49 mother tongues. *Plos One*. 10(11).

Wang, C. (2004). Self-regulated learning strategies and self-efficacy beliefs of children learning English as a second language, Doctoral Dissertation, Ohio State University

White, L. (1959). *Motivation considered the concept of competence*. NewYork: Rockvillepike

Whiteley, W.H. (1969). Swahili*: The Rise of National Language*. London: Methuen.

Widdowson, Henry G. (1973). An applied linguistic approach to discourse analysis (Unpublished PhD dissertation). Edinburgh: University of Edinburgh.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili,* Dar-es Salaam, Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2011). *Sera ya Elimu*. Dar-es Salaam, Tanzania.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Dar-es Salaam, Tanzania.

Wizara ya Elimu na Utamaduni, (1996), Muhtasari wa Kiswahili. Dar-es Salaam, Tanzania.

Wizara ya Elimu na Utamaduni, (1997). *Sera ya Utamaduni*. Dar-es Salaam, Tanzania.

Wizara ya elimu sayansi na teknolojia (2016). *Muhtasari wa somo la Kiswahili*, Dar-es Salaam, Tanzania.

Wright, M. (1999). Influences on learner attitudes towards foreign language and culture. *Educational Research*, 41, 197-208

Yoradi S.Y. (2013). Lugha ya Kiswahili katika Kufundishia na Kujifunzia Elimu Shuleni na Vyuoni. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (M.A. Kiswahili), Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Zhou, M. and Sun, H. (2004**).** *Language Policy in the People's Republic of China: Theory and Practic Since 1948* [http://www. utwente. nl/cw/ theorieen overzicht/ theory].